# Nipashe

Jumatatu Oktoba 12, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580366

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11

**ALIYEUA** mke naye ajichoma kwa kisu

UKURASA 3



**JELA** maisha kwa kunajisi mtoto wa shemeji

UKURASA 3

# CHADEMA: Hatuna kinyongo na Magufuli

UKURASA 2



Mgombea mwenza wa urais kupitia (CHADEMA), Salum Mwalim, akihutubia mkutano wa kampeni katika eneo la Kihesa Sokoni, mjini Iringa juzi.
**PICHA: FRANCIS DANDE**

# Cheyo asisitiza kumuunga mkono mgombea wa CCM

UKURASA 2




Mgombea mwenza wa urais kupitia CCM, Samia Suluhu Hassan, akiteremka kutoka kwenye helikopta 5Y-HSN ya chama hicho, alipowasili katika kijiji cha Kalakala Jimbo la Kwela, Sumbawanga Vijijini mkoani Rukwa jana, kwa ajili ya kampeni.
**PICHA: OMR**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

### ZITTO ARUHUSIWA, KUREJEA KAMPENI

KIONGOZI Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ametoka hospitali ...

**UKURASA WA 4**

### TAMWA YAOMBA SERIKALI UTARATIBU ULINZI WA WATOTO

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimeomba serikali...

**UKURASA WA 4**

### SARATANI BADO TISHIO NCHINI

TAASISI ya Tiba ya Saratani Ocean Road (ORCI), imebainisha kuwapo na ongezeko la wagonjwa wapya kila mwaka zaidi ya...


**Vichwa saba vya treni vyazinduliwa**

UKURASA 3

**MICHEZO** KIDUKU AMWANZISHIA MTHAILAND DOZI KUTWA MARA TATU UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

## Lissu ataka Watanzania kujitokeza Oktoba 28

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi kupiga kura kwa kiongozi wanayeona anafaa kuliongoza taifa la Tanzania kwa miaka mingine mitano.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye mikutano tofauti ya kampeni mkoani Singida, na kuwataka Watanzania wafanye maamuzi sahihi Oktoba 28, mwaka huu, kwa ajili ya maendelo yao.

"Sauti ya watu ni sauti ya Mungu na yenu kwenye uchaguzi huu, itakuwa sauti ya Mungu, hakuna atakayeweza kupambana na Mungu, mkiamua, Tanzania mkiamua hakuna atakayewabishia," alisema.

"Mkapige kura, kila mmoja wetu ili tukomboe nchi yetu, tukapige kura, tukomboe nchi yetu, tukapige kura tutendewe haki, jambo la kwanza ni kwenda kupiga kura ya kimbunga," alisisitiza Lissu.

Akiwa wilayani Ikungi juzi, Lissu alisema ilani ya chama hicho, inaeleza kuwapo kwa uhuru na haki na maendeleo kwa wananchi.

Aidha, alilaani mauaji ya viongozi mbalimbali wa chama hicho na hatua kutochukuliwa na hata zikichukuliwa wanakamatwa viongozi wa chama hicho, wakati upande mwingine ni tofauti.

Alisema Oktoba 6, mwaka huu, kuuawa kwa aliyekuwa Katibu Mwenezi wa CHADEMA Kata ya Mhintiri, Jimbo la Singida Magharibi, Nicholas Andrea, ikidaiwa kukutwa amekatwa mapanga na alizikwa juzi.

"Mungu anafahamu tumekuwa tukionewa na Jeshi la Polisi wanasema wajibu wao ni kulinda raia, lakini hawalindi, hawasimamii viapo vyao," alisema.

Akiwa Mkalama na Iguguno, Lissu alisema ataongoza serikali ya haki na maendeleo yenye maana kwa wananchi wa kawaida, ikiwamo kuhakikisha dawa kwenye hospitali, huduma bora za maji, shule na barabara.

"Tuchague serikali itakayolinda uhuru wetu, itakayosimamia haki zetu, itakayoleta maendeleo ya watu wetu na si kunyanyasa watu hadharani, tusilalamike tu bali tuchukue hatua kwa kupiga kura," alisema.

## Zitto atoka hospitali, kurejea kampeni

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ametoka hospitali na kuwashukuru wahudumu wa afya sehemu alizotibiwa, huku akiahidi kurudi kwenye kampeni za uchaguzi mkuu.

Jana katika ukurasa wake wa Tweeter aliandika: "Nimeruhusiwa kutoka hospitali. Nawashukuru madaktari na wauguzi Kituo cha Afya Kalya-Uvinza, Hospitali ya Maweni Kigoma na Hospitali ya Aga Khan Dar es Salaam.

"Asanteni sana wote kwa dua, sala na maombi yenu. Natarajia kurudi kwenye kampeni siku chache zijazo," alisema ambaye anatetea nafasi yake ya ubunge Jimbo la Kigoma Mjini.

Katika ukurasa wa mke wa Zitto, unaojulikana kwa jina la Binti Bwana, aliandika: "Zitto alivunjika bega kwenye ajali ya juzi Kigoma (Oktoba 8) amefanyiwa operesheni kurekebisha bega hilo. Tunashukuru operesheni imeenda salama. Ameniomba niwashukuru wote kwa maombi."

Zitto alipata ajali Oktoba 6, mwaka huu, mpakani mwa kata za Kalya na Lukoma, mkoni Kigoma.

Oktoba 10, mwaka huu, Mgombea ubunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Fuata Nabaraka, alipata ajali akiwa na wenzake saba, ambao wajeruhiwa na baada ya matibabu wanne waliruhusiwa kutoka hospitali.

Ajali hiyo ilisababishwa na hitilafu kwenye mfumo wa breki za gari hilo lililoshindwa kupanda mlima.



Rais mstaafu Alhaj Ali Hassan Mwinyi (katikati), akikata utepe kuzindua kitabu cha "Kwa nini Amani?", kilichoandikwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Al-Hikma, Sheikh Nurdeen Kishk (kulia), katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Rais wa Taasisi hiyo, Abdulqadir Al-Ahdal na (wa pili kushoto) ni Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CHADEMA: Hatuna kinyongo na Magufuli

**Na Francis Godwin,** IRINGA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeahidi kikishinda uchaguzi na kuingia madarakani, hakitakuwa na kinyongo na Rais Dk. John Magufuli, kwa kuwa kitampa kazi ya kufanya.

Pia, kimesema kitampa nafasi ya kwenda nje ya Tanzania zikiwamo nchi za Ulaya kumwakilisha, Tundu Lissu ambaye wakati huo atakuwa rais.

Akihutubia wananchi katika viwanja vya Kihesa Sokoni, mjini hapa, mgombea mwenza wa urais kupitia chama hicho, Salum Mwalimu, alisema kiongozi huyo asiwe na wasiwasi kwa kuwa bado atafanyakazi na serikali ya chama chao.

Alifafanua kuwa Lissu hataunda serikali ya kinyongo na kulipa kisasi kwa kiongozi yeyote wa serikali iliyotoka madarakani, badala yake atawapata nafasi ya kufanya kazi pamoja.

Akizungumzia serikali ya CHADEMA, mgombea mwenza huyo alisema, itawaenzi vyema viongozi hao akiwamo rais anayemaliza muda wake (Magufuli), mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya.

Pia, aliwatoa wasiwasi wakuu vya vyombo vya ulinzi na usalama nchini, likiwamo Jeshi la Polisi kuwa serikali ya CHADEMA itahakikisha wanaishi kwa uhuru.

"Hatuna shida na Dk. Magufuli, tukiingia madarakani tutaendelea kumpa heshima yake ya kulitumikia taifa kwa kutumwa kwenye shughuli mbalimbali za kitaifa katika vikao vya nje, asiwe na hofu, suala la kula bata atakula sana bata wakati wa serikali ya CHADEMA," alijinadi Mwalimu kwa wananchi hao.

Kuhusu uhuru wa vyombo vya habari, alisema serikali ya CHADEMA ikishaingia madarakani itapeleka bungeni marekebisho ya miswada yote ya sheria.

## Cheyo: UDP inamuunga mkono mgombea urais CCM

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama cha United Democratic Party (UDP), John Cheyo, amesisitiza msimamo wa chama chake kumuunga mkono mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, uko pale pale.

Cheyo aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa UDP haijabadili msimamo wake katika suala hilo.

"Hatujasitisha kumpigia kampeni mgombea urais wa CCM, tulikubaliana kwenye chama endapo CCM kitamsimamisha Rais Magufuli kuwa mgombea urais tutamuunga mkono, tunaona hapa katikati kuna baadhi wamesema tumesitisha msimamo huu, hatujasitisha huu ndiyo msimamo wa UDP," alisema.

Cheyo alisema mambo ya uchaguzi ni hiari ya mtu kumpigia kampeni nani. Alisema walitangaza kumuunga mkono mgombea urais wa CCM na hawajafanya mazungumzo yoyote na chama hicho bali wamevutiwa na utendaji kazi wake wa kuimarisha miundombinu.

Alisema hawajavunja sheria yoyote kumuunga mkono mgombea wa CCM.

"UDP inaendelea na msimamo ule ule, tumeshuhudia namna Rais Magufuli amefanya mambo makubwa, miaka mingi katika nchi hii imezungumza kuhusu kujitegemea na ni kipindi hiki tu tumeona raha ya kujitegemea, tumeona uhuru bila kutegemea mtu, rais tuliyenaye ametuonyesha kama tukikusanya rasilimali vizuri sisi ni matajiri hatuhitaji utegemezi wa kujenga miradi mikubwa kwa kutaka misaada tunaweza wenyewe.

"Jana nimeenda kuona mradi wa Ubungo amefanya makubwa, Watanzania tupo huru hatuhitaji Muingereza."

Alisema sababu nyingine ya kumuunga mkono mgombea wa CCM ni namna alivyoimarisha miundombinu ambayo mikoa mbalimbali inatumia kusafirisha mazao.

Alisema sababu nyingine ni utekelezaji wa miradi wa reli ya kati ambao wanaona wasiopomuunga mkono haitajengwa.

"Tunahitaji umeme kuchenjua dhahabu zetu, kuendesha viwanda ili kuongeza ajira, UDP tunafanya kampeni ili kuunga mkono miradi iliyopo sasa," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Mume ajichoma kisu tumboni tuhuma za kuua mke

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia Paulo Shija (30), mkazi wa kijiji cha Didia wilayani Shinyanga, kwa tuhuma za kumuua mkewe Mariam Julius (26) kwa kumchoma kisu shingoni na yeye mwenyewe kujaribu kujiua kwa kujichoma kisu tumboni na kusababisha utumbo wake kutoka nje.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema tukio hilo limetokea usiku wa kumakia jana, majira ya saa saba usiku, wakati Mariam akiwa amelala na mumewe na kuzuka ugomvi ambao mtuhumiwa alikuwa akimtuhumu mkewe kuwa na mwanaume mwingine anayetoka naye kimapenzi.

Alisema ugomvi huo uliendelea na mtuhumiwa alichukua kisu na kumchoma shingoni mkewe na kusababisha kifo chake.

Alisema mtuhumiwa alipoona hali hiyo, naye alichukua kisu akijaribu kujiua kwa kujichoma tumboni na kusababisha utumbo wake kutoka nje na kukimbizwa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga kupatiwa matibabu.

"Chanzo cha kifo cha mwanamke huyu Mariam Julius ni wivu wa kimapenzi, mume wake alikuwa akimtuhumu ana mahusiano ya kimapenzi na mwanaume mwingine ambaye hamjui jina wala sura, na kudai kuna watu (akiwataja kwa majina) walikuwa wakimtafutia wanaume," alisema Magiligimba.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhia maiti, huku mtuhumiwa akipatiwa matibabu kwenye hospitali hiyo, na kwamba hali yake ni mbaya.

Kamanda alitoa wito kwa wanandoa kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi, badala yake wapeleke matatizo yao kwenye ofisi za dawati la jinsia na watoto, viongozi wa dini, pamoja na ofisi za ustawi wa jamii, ili kupata suluhisho la migogoro yao.

# Vichwa vya treni vya bil. 13/- vyazinduliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezindua vichwa saba vya treni kwa ajili ya mizigo vilivyofanyiwa matengenezo katika karakana ya Shirika la Reli Nchini (TRC) mkoani Morogoro viliivyogharimu kiasi cha Sh. bilioni 13.

Akizindua vichwa hivyo jana jijini Dodoma, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema vitasaidia kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

Kamwelwe, alisema kuwa vichwa hivyo saba vimekarabatiwa kwa gharama ya Sh. bilioni 13 ikiwa ni fedha kutoka Benki ya Dunia mkopo wenye masharti nafuu.

"Ukarabati wa vichwa hivi vya treni kwa ajili ya mizigo ni sehemu ya mradi wa kuboresha reli ya kati ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia utakao gharimu kiasi cha Sh. bilioni 680," alisema Kamwelwe. Alisema kuwa katika mradi huo pia utahusisha shughuli za ukarabati wa njia ya reli, ukarabati wa vichwa vya treni pamoja na mabehewa ya mizigo.

Pia Kamwele alisema kuwa ukarabati wa vichwa hivyo utasaidia kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka katika Bandari Kavu ya Kwara na vingine vitapelekwa mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Saalam.

"Awali hatukuwa kabisa na vichwa hivi kwa ajili ya mizigo hali ambayo ililazimika kutumia vichwa vikubwa kuvuta mizigo hali ambayo inachangia gharama kubwa za uendeshaji," alifafanua Kamwele. Vilevile, alisema katika mwaka huu wa fedha wametenga kiasi kingine cha fedha kwa ajili ya kukarabati vichwa vingine saba ambavyo vitakuwa kwa ajili ya mizigo.

"Hii inamaanisha kuwa serikali ya awamu ya tano imedhamilia kuboresha Shirika la Reli Nchini kwa kuboresha miundombinu mbalimbali na ukarabati huu umefanywa na Watanzania," alisema.

Vilevile alisema kuwa kufanya ukarabati wa vichwa hivyo kumesaidia kupunguza gharama kwa serikali kwa kuwa kama ingenunua vipya kila kimoja kingegharimu Sh. bilioni 4.

Akizungumzia ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) unaendelea, alisema kuwa mwezi Februari 2021 serikali itaanza kupokea mabehewa kwa ajili ya usafiri huo.

Hata hivyo, alitoa rai kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuwasimamia makandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali ili ujenzi kufanyika kwa wakati.




Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (kulia), akipokea msaada wa pedi za wanafunzi wa kike kwa ajili ya shule mbalimbali za wilaya hiyo, kutoka kwa Meneja Uhusiano wa kampuni ya IPP, Nancy Mwanyika, katika hafla iliyofanyika Shule ya Sekondari Minaki jana, baada ya matembezi ya hisani yaliyoandaliwa na EATV/Radio kupitia kampeni yake ya Namthamini kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Kike Duniani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jela maisha kwa kunajisi mtoto wa shemeji yake

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Mnolela, wilayani Lindi, Ramadhani Yusufu (22), amehukumiwa kwenda jela maisha, baada ya kukutwa na hatia ya kumlawiti mtoto wa kike wa shemeji yake mwenye umri wa miaka mitatu.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Lindi, Maria Batraine, baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote ikiwamo mshtakiwa kukiri kosa hilo.

Awali, Hakimu Batraine alitoa nafasi kwa mshtakiwa kujitetea, ambaye aliiomba Mahakama imwonee huruma kwa kutompa adhabu kubwa kwa kuwa alifanya kitendo hicho kimetokana na kubanwa na ibilisi wa mapenzi.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, aliiomba Mahakama kumpatia mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

Aidha, Mramba alitaka Mahakama kuzingatia kuwa kitendo alichofanyiwa mtuhumiwa ni cha kinyama zaidi dhidi ya mtoto asiyekuwa na hatia.

Akitoa hukumu hiyo, Batraine alisema kutokana na kosa alilolifanya mshtakiwa kuwa na ukomo wa kifungo, alimuhukumu kutumikia gerezani kifungo cha maisha.

Awali, ilidaiwa mahakamani kuwa mshtakiwa kwa makusudi, huku akitambua anachokifanya ni kosa, Septemba 17, mwaka huu, katika Kijiji na Kata ya Madangwa alimlawiti mtoto wa shemeji yake mwenye umri wa miaka mitatu.

Kwa mujibu Mramba, unyama huo dhidi ya mtoto huyo alimsababishia maumivu makali maeneo mbalimbali ya mwili wake zikiwamo za siri.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA ILIYOPO DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 42 YA 2016**

**CATHERINE HONORATI............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **CRDB BANK PLC**
2. **METHOD KAUNGA MORIS**
3. **HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE – POPOTE ALIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la rufaa ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama ya Rufaa hapa Dar es salaam tarehe 19/10/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00) katika ukumbi wa Mahakama ya Biashara. Unapaswa kuhudhuria siku ya tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi yako yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

**Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 1/10/2020**

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

E. G. Mrangu
Kny: **MSAJILI**
**MAHAKAMA YA RUFANI**

115938502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA ILIYOPO DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 42 YA 2016**

**CATHERINE HONORATI..........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **CRDB BANK PLC**
2. **METHOD KAUNGA MORIS**
3. **HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: METHOD KAUNGA MORIS – POPOTE ALIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la rufaa ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama ya Rufaa hapa Dar es salaam tarehe 19/10/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00) katika ukumbi wa Mahakama ya Biashara. Unapaswa kuhudhuria siku ya tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi yako yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

**Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 1/10/2020.**

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

E. G. Mrangu
Kny: **MSAJILI**
**MAHAKAMA YA RUFANI**

115938502

# DC atishia kufunga mgodi wa dhahabu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

SERIKALI imetishia kuufunga mgodi wa dhahabu wa Bulumbaka ulioko katika kijiji cha Gasuma, Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu kutokana na uwapo wa migogoro ya mara kwa mara ambayo inasababishwa na makundi ya wachimbaji. Hatua hiyo imekuja kutokana na kusimama kwa muda wa siku mbili shughuli za uchimbaji kwenye mgodi huo, kutokana na mgogoro wa kiuongozi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Festo Kiswaga, alisema serikali haitavumilia migogoro hiyo katika mgodi.

Kiswaga alisema wamepata taarifa kuwa baadhi ya watu kwenye mgodi huo wanaanzisha vurugu kwa lengo la kutaka kutorosha madini usiku, na kwamba serikali haitavumilia hali hiyo. Katika hatua nyingine Kiswaga amewapiga marufuku ya kuingia katika mgodi huo, baadhi ya wachimbaji ambao wanatajwa kusababisha migogoro hiyo, ambapo Jeshi la Polisi ambalo linaongoza ulinzi mgodini hapo, limeagizwa kuhakikisha linawazuia wasifike mgodini hapo.

"Uongozi wa Mkoa na Wilaya uliwasikiliza wote wanaolalamika na wale wanaolalamikiwa na kusuluhusisha... sisi tulifikiri mambo sasa yako vizuri, lakini tunashangaa bado yanaendelea, kama serikali hatutakubali mtu yeyote atuyumbishe na kuchochea migogoro hii," alisema Kiswaga.

"Tumeliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha wale wote ambao wanatajwa kuchochea vurugu hizi, kuwazuia wasifike kwenye mgodi, tumewapiga marufuku kama wana shughuli yoyote hapa mgodini watume wasaidizi wao," aliongeza Kiswaga.

Wakiongea na waandishi wa habari mgodini hapo, baadhi ya wachimbaji walisema chanzo ni wamiliki wa mashamba kuzuia shughuli za uchimbaji kutokana na kutounga mkono uongozi ambao umechaguliwa kuongoza mgodi. Matinde Ntudu, mmoja wa wamiliki mashamba, alisema uongozi ambao ulichaguliwa na serikali hauna uwezo wa kuendesha mgodi, kwani historia yake inaonyesha walisababisha mgodi namba moja kuharibika.

Naye Nkamba Lisu mmiliki wa mashamba, alisema kuwa uongozi ambao umechaguliwa hawautaki kwani katika mgodi namba mmoja ambao waliharibu waliacha madeni mengi ambayo hawajalipa wakiwamo watu wa usafi.

Kaimu Ofisa Madini Mkoa, Oscar Kaloa, alisema malalamiko hayo yalifanyiwa kazi katika kikao cha pamoja kati ya Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, na vikundi vyote vilivyoko kwenye mgodi huo. Alisema wamiliki wa mashamba kwenye kikundi ambacho kilichaguliwa kuongoza mgodi, wao walipewa nafasi ya mwenyekiti, naibu katibu pamoja na naibu mhasibu tofauti na mwanzo wao hawakuwamo.

"Kwenye kile kikao mkuu wa mkoa aliagiza wananchi wa kijiji ambacho mgodi upo ndiyo wapewa tenda ya kuongoza mgodi, maana mwanzoni walikuwa wamepewa tenda watu kutoka maeneo mengine, ndipo wamiliki wakapewa hizo nafasi na mgogoro ukamalizika," alisema Mhandisi Kaloa.

# Zaidi ya 42,000 waugua saratani kila mwaka

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Saratani Ocean Road (ORCI), imebainisha kuwapo na ongezeko la wagonjwa wapya kila mwaka zaidi ya 42,060.

Mkurugenzi wa Tiba wa ORCI, Dk. Mark Mseti, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa Siku ya Tiba Shufaa Duniani ambayo huadhimishwa Oktoba 10 kila mwaka yenye kauli mbiu inayosema, 'Huduma Yangu Faraja Yangu'.

Alisema idadi hiyo ya wagonjwa inaongezeka kila mwaka, na kwamba kati ya wagonjwa hao asilimia 70 hadi 80 wanafika hospitalini hapo wakiwa hatua za juu za ugonjwa na asilimia 20 hadi 30 wanafika wakiwa katika hatua ya kwanza na ya pili ya kutibika.

Alisema wagonjwa wanaofika katika hatua ya tatu hadi ya nne, matibabu yao huwa ya kuzuia kuenea kwa saratani na kumwongezea siku za kuishi tofauti na hatua ya kwanza na ya pili ambayo mgonjwa hupatiwa matibabu na kupona.

"Asilimia 70 hadi 80 ya wagonjwa tunaowaona wanahitaji huduma ya tiba shufaa kwa hali moja au nyingine kwa sababu wanakuwa katika hali mbaya ya ugonjwa," alisema daktari huyo bingwa.

Akizungumzia matibabu shufaa wanayotoa katika taasisi hiyo, alisema tiba shufaa ni huduma ambayo anapatiwa mgonjwa mwenye magonjwa endelevu kama vile saratani.

"Lengo ni kuboresha maisha ya wagonjwa na familia yake, kama ana maumivu makali tutahakikisha tunampunguzia maumivu, tunampa faraja, tunamwondoa kwenye changamoto zote zinazomkabili mgonjwa wetu," alisema Dk. Mseti.

Alisema wagonjwa wenye magonjwa yasiyoambukiza kama saratani ndio walengwa wakuu na huwapa huduma za kisaikolojia, kisheria na ushauri wa namna ya kuendesha maisha mara baada ya kupata ugonjwa.

Alisema wagonjwa wa aina hiyo pia wanahitaji ushauri wa kifedha na kuendesha maisha ili kumudu matibabu mengine wanayopatiwa.

"Wagonjwa hawa pia wanahitaji huduma za kiroho kutoka kwa viongozi wa dini, ili wajisamehe makosa yao na wasiwe watu wa kujihukumu kutokana na ugonjwa walionao," alisema Dk. Mseti.

Akizungumzia mafanikio ya miaka mitano ya taasisi hiyo, alisema wameongeza idadi ya watoa huduma, wamepata mashine za kisasa na dawa za kutosha ambazo zinawapa uhakika wa matibabu kwa wagonjwa wao.



Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shy-Rose Bhanji, akimnadi mgombea urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli, katika maeneo mbalimbali ya Mbweni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA yaomba serikali utaratibu ulinzi wa watoto

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimeiomba serikali kuandaa utaratibu wa ulinzi, utoaji taarifa na ufuatiliaji kwa watoto wakati wa magonjwa ya mlipuko kama ilivyotokea corona, ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe, kuhusu maadhimisho ya kimataifa ya mtoto wa kike chini ya kaulimbiu ya kitaifa: "Tumwezeshe mtoto wa kike, kujenga taifa lenye usawa" na ya kimataifa: "Sauti yangu, ni mustakabali wetu wa usawa", siku hiyo huadhimishwa kukumbuka madhila wanayopitia watoto wa kike na kuikumbusha jamii nguvu iliyomo kwa watoto.

Kwa mujibu wa Shebe, tangu kuzuka kwa ugonjwa wa corona, unyanyasaji wa nyumbani umeongezeka kwa kasi, na kuiasa jamii kuacha mifumo inayomkandamiza mtoto wa kike ili kuwa na taifa lenye amani linalozingatia ulinzi kwa watoto wa jinsia zote.

Alisema takwimu za uhalifu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), zinaonyesha katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2016, jumla ya kesi 10,551 za uhalifu dhidi ya watoto ziliripotiwa katika vituo vya polisi.

Pia, alisema hiyo ikilinganishwa na kesi 9,541 kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2015, ikiwa ni uhalifu wa ubakaji, ukeketaji wa watoto, wizi wa watoto, utekelezaji na mashambulio ya kudhuru mwili.

"TAMWA tunaomba wazazi, walezi na watoto wa kike wanaofanyiwa ukatili, wavunje ukimya, kwani zipo asasi, taasisi na vyombo vya serikali ambavyo wanaweza kuvitumia kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia," alisema Shebe na kuongeza;

"Tunasisitiza serikali ijenge mifumo imara ya utoaji taarifa ili tujue kwa kina sababu na kiwango cha ukatili huu...tukumbuke watoto ni taifa la kesho, wanapoharibiwa misingi bora ya maisha, tunakwenda kuharibu mustakabali wa taifa."

Alikumbusha umuhimu wa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, kwa kuamiani kuwa mtoto wa chini ya miaka 18 bado hajapevuka vya kutosha kumudu majukumu ya ndoa na kubeba ujauzito.

Vile vile, alimpongeza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kwa jitihada za ulinzi na afya kwa watoto wa kike nchini.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF), linaeleza watoto wa kike milioni mbili huolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 kila mwaka.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, watoto wa kike takribani milioni sita hadi 17 duniani hawajapata nafasi ya kwenda shule na wa kike milioni 15 duniani wa kuanzia miaka 15 hadi 19 wameathirika kisaikolojia kutokana na manyanyaso ya ukatili wa kijinsia kama kubakwa, vipigo na udhalilishaji wa kingono.

HABARI KITAIFA

# Prof. Kitila kukomesha maiti kudaiwa hospitali

**Na Thobias Mwanakatwe**



MGOMBEA ubunge Jimbo la Ubungo kupitia CCM, Prof. Kitila Mkumbo (pichani), ameahidi kwamba iwapo atapewa ridhaa, atahakikisha malalamiko ya wananchi ya kutozwa huduma ya kuchukua miili ya marehemu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili- Mloganzila tatizo hilo linakomeshwa haraka.

Alitoa ahadi hiyo jana, wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Makukumila kwenye mfululizo wa kampeni zinazoendelea katika jimbo hilo kuwaomba wananchi kuichagua CCM.

Prof. Mkumbo alisema msingi wa kwanza wa CCM ni utu, hivyo kuzuia kuchukua mwili wa marehemu inaenda kinyume cha msingi wa chama hicho.

"Serikali ya CCM itakakikisha tatizo hilo linakoma haraka sana, na tayari nimeshaanza kuongea na Waziri na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuangalia namna ya kukomesha tatizo hilo," alisema.

Alisema hata leo atamweleza Rais John Magufuli, wakati wa mkutano wa kampeni utakaofanyika katika Jimbo la Ubungo.

Prof. Mkumbo alisema suala jingine ambalo linalalamikiwa na wananchi dhidi ya Hospitali ya Mloganzila ni kuwatoza fedha wanawake wanapokwenda kujifungua.

Alisema kwa mujibu wa sera ya taifa, huduma za kujifungua zinatakiwa ziwe bure, hivyo kuwatoza wanawake fedha ni kwenda kinyume cha sheria.

"Jambo hilo halikubaliki, hatuwezi kuruhusu na Rais Magufuli, nami nimelichukua, tutalifuatilia ili kuhakikisha wataalamu wa afya wanafuata utaratibu...huduma za kujifungua kwa kinamama zinakuwa bure," alisema.

Prof. Mkumbo aliwahidi wananchi kwamba kituo kidogo cha Polisi Makulumila kilichojengwa atazungumza na viongozi wa Jeshi la Polisi ili kiweze kuwa na askari muda wote, kwa lengo la kudhibiti vitendo vya uhalifu.

# LHRC yawapa kazi wabunge watarajiwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimewaomba wabunge watakaochaguliwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kulipa kipaumbele suala la kufutwa kwa sheria ya adhabu ya kifo kwa sababu haitekelezeki nchini. Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema hayo jana kwenye Siku ya Kupinga Sheria ya Kunyongwa Duniani iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema adhabu hiyo haina umuhimu kwa sababu kwa Tanzania kwa zaidi ya miaka 20 hakuna mtu aliyehukumiwa kifo aliyewahi kunyongwa.

"Hatusemi wanyongwe, ila ni adhabu ambayo haitekelezeki, hata Rais wa sasa wa awamu ya tano alishasema yeye hataki kabisa kusaini adhabu ya kifo, kwa hiyo ni kitu ambacho haitekelezeki, haina haja ya kuwapo katika sheria zetu za Tanzania," alisema.

Alisema ni rahisi kuifuta sheria ya kifo kwa sababu kama haijatekelezwa kwa zaidi ya miaka 20, hivyo tunaziomba mamlaka za utungaji sheria zifikirie kuifuta katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lijalo.

Aliongeza kuwa kwenye magereza kuna watu takribani 400, ambao wameshahukumiwa kifo, lakini tu husubiri kunyongwa, lakini haitekelezwi, jambo ambalo ni kuwapotezea muda wao na kunyimwa fursa ya kuwa na familia zao.

"Kwanza ni hasara kwa taifa kwa sababu unawalisha watu 400 ambao hawafanyi kazi, wanaendelea kuwapo gerezani tu, ni adhabu isiyokuwa na maana kabisa," alisema.

Alisema LHRC ilishawahi kufungua kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kutaka suala la adhabu ya kifo lifutwe.

Alisema LHRC ilishinda kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, ambapo serikali iliagizwa ifute adhabu hiyo.


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe | Nipashe mwendo mdundo

Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)

PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
Download on the App Store | GET IT ON Google Play

KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz | nipashe | TheGuardiantz | YouTube TheGuardiantz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali isiishie Taifa Stars, ihudumie timu zote za Taifa

**BAADA** ya kuhudumiwa kwa tabu kwa muda mrefu, hatimaye sasa ni faraja kwa timu ya Taifa ya Soka ya Tanzania, Taifa Stars, furaha hiyo ikitokana na serikali kutangaza kutenga bajeti rasmi ya mwaka mzima kwa timu hiyo. Kwa muda mrefu Taifa Stars kama zilivyo timu nyingine za michezo mbalimbali za Taifa hapa nchini, jukumu la kuihudumia limekuwa likiachwa chini ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), jambo ambalo lilikuwa mzigo mzito kwa shirikisho hilo. Hatua hiyo iliifanya TFF kutembeza bakuli mara kadhaa pindi Taifa Stars inapokabiliwa na mashindano mbalimbali ama mechi za kimataifa za kirafiki, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa hapo awali lilikuwa likichangia wachezaji kutokuwa na ari ya kuvutiwa kwenda kuitumikia timu hiyo pindi wanapoitwa.

Lakini wiki iliyopita, wakati wa hafla fupi ya TFF na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), ya kuingia mkataba wa wenye thamani ya Sh. bilioni tatu kwa ajili ya kuidhamini Taifa Stars, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, aliweka wazi kuwa kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania sasa timu hiyo imetengewa bajeti yake na serikali.

Hii ni hatua ya kupongezwa sana kwa serikali hii ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli, kwani imeonyesha ni kwa namna gani imedhamiria kuona Tanzania inafanya vizuri katika medali ya soka, ambayo kwa sasa ni ajira kubwa kwa vijana. Ingawa katika hilo, tunatambua Tanzania itakuwa imechelewa sana, kwani mataifa mengi yaliyopiga hatua kisoka na michezo kwa ujumla, jukumu la kuzihudumia timu za taifa ni la serikali, lakini bado tuna kila sababu ya kumpongeza Rais Magufuli kwa kuliona hilo na kuridhia serikali yake kuanza kubeba jukumu hilo.


Pamoja na pongezi hizo, lakini Nipashe hatuna budi kuikumbusha serikali, isiishie kufanyika kwa Taifa Stars ama soka pekee, bali tungetamani kuona ikibeba jukumu kama hilo kwa timu zote za taifa za michezo mbalimbali nchini kama ambavyo zinafanya nchi zilizopiga hatua katika medali ya michezo.

Mara kadhaa, tumeshuhudia timu za Taifa za riadha, ngumi, tenesi, mpira wa pete na michezo mingine zikitembeza bakuli ili kuweza kwenda kushiriki michuano mbalimbali ya kimataifa kwa vipindi tofauti, hivyo ni wakati sasa wa serikali kugeukia timu zote za taifa ili kuinua sekta ya michezo nchini kwa ujumla.

Tunatambua huo ni mzigo mzito, lakini kwa kuanza serikali haina budi kutenga hata bajeti ndogo kwa timu zote za taifa za michezo mbalimbali, na si soka pekee ili kuvipunguzia mzigo vyama ama mashirikisho ya michezo husika ambayo huwa katika wakati mgumu pindi wanapokabiliwa na michuano mbalimbali nje ya nchi. Aidha, pamoja na serikali kuamua kuanza kuihudumia Taifa Stars, tunaikumbusha TFF hiyo isiwe sababu ya idara yao ya masoko kulala na kuona tayari imeshatua mzigo huo, badala yake huu sasa ndio uwe wakati muafaka wa kupanua idara ya masoko na kuipa nguvu ya kuingia sokoni zaidi kuongeza wadhamini wa timu hiyo na zingine. Nipashe tunatamani kuona TFF ikizidi kuzishawishi kampuni nyingi zaidi kujitokeza kuomba kuidhamini Taifa Stars na timu nyingine ikiwamo Twiga Stars na Serengeti Boys, kwani tunatambua wadhamini wanapokuwa wengi na maslahi ya wachezaji wanaoitwa kuzitumikia timu hizo yanakuwa makubwa, hivyo kuwafanya wahamasike na kuongeza ushindani ili kuweza kujumuishwa katika vikosi hivyo. Tunatamani kuona wachezaji wanapigana vikumbo kwa kuonyesha uwezo mkubwa uwanjani ili kujitengenezea nafasi ya kuitwa timu ya taifa, jambo ambalo litaifanya Tanzania kuwa na timu imara za taifa.

Ili hilo lifanyike kwa ufanisi mkubwa, mbali na wachezaji kuona fahari kuitwa kuichezea timu ya taifa, lakini mazingira mazuri na maslahi makubwa kwao ni miongoni mwa vitu ambavyo vitawaongezea hamasa kubwa na kuwafanya kuongeza juhudi wawapo uwanjani. Tunaamini serikali itasikia kilio chetu cha kuimulika michezo mingine, lakini ni wakati wa TFF kuzidi kushawishi kampuni nyingi zaidi kujitokeza kutoa udhamini wao kwa timu za taifa na wakati huo huo wachezaji wakiona umuhimu wa kuitendea haki jezi ya taifa pindi wanapoitwa kuitumikia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Mzimu wa Lusajo umeanza kuitafuna Namungo taratibu

**NIMESIKIA** kuwa uongozi wa Namungo umekaa kikao na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hitimana Thiery kuzungumza naye kuhusu mwendo wao wa kusuasua kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21. Kumbuka kuwa Namungo hiyo hiyo ndiyo inayotarajiwa kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, ambapo ratiba yake huenda ikatoka mwezi ujao.

Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu, amesema kwa namna ambavyo kikosi chao kinakwenda kwenye ligi imewalazimu kukaa chini na kuzungumza na benchi la ufundi.

"Tulianza kukaa kikao na uongozi wenyewe na kisha tulimwita kocha tukazungumza naye tukiwa na benchi lote la ufundi ili kujua tatizo lipo wapi?" Alisema mwenyekiti huyo. Alisema ni kweli msimu huu haujaanza vizuri kama ilivyokuwa uliopita na sababu kubwa ni kwamba safari hii maandalizi yamekuwa mafupi kutokana na ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na vrusi vya corona. Akaongeza kuwa jambo hilo si lao peke yao, kwani timu nyingi zimekuwa zikikumbana na hali kama yao, lakini wamejipanga kuona wanarejea kwenye ubora wao.

Sitaki kujua sana ni nini walichoongea uongozi na kocha wao, lakini chochote ambacho wameongea ni lazima timu hiyo irejee kwenye kiwango chake kilichozoeleka ili isiende kutia aibu kwenye michuano ya kimataifa. Kwenye Ligi Kuu msimu huu, Namungo bado haijafanya vema tofauti na msimu uliopita ilipoanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza. Imecheza mechi tano mpaka sasa, ikiwa imeshinda mbili na kufungwa tatu. Imefunga mabao mawili tu na kufungwa matatu. Inashikilia nafasi ya tisa kwa kuwa na pointi sita.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, Namungo imepoteza mechi mbili nyumbani, ikiwa Uwanja wa Majaliwa, Rungwa mkoani Lindi, kati ya mechi tatu ilizocheza. Ilikuwa si rahisi kuona Namungo ikipoteza nyumbani msimu uliopita. Ilipoteza mara moja tu dhidi ya Coastal Union. Wengi wanajiuliza ni nini kimeikumba Namungo msimu huu? Ukweli ni kwamba vikao vitakaliwa, lakini binafsi naona kuwa lilikuwa ni kosa kubwa na la kiufundi ililofanya Namungo kumuacha straika wao Reliants Lusajo kuondoka kirahisi kwenye klabu hiyo bila kutavuta mtu sahihi wa kuvaa viatu vyake.

Sijui nini kilitokea, lakini Lusajo aliondoka kwenye klabu hiyo na kujiunga na KMC ya Kinondoni. Sidhani kama kweli Namungo ingetaka kumbakisha Lusajo ingeshindwa. Nasema lilikuwa ni kosa kubwa la kiufundi kwa sababu huwezi kumuacha straika aliyeongoza kwenye ufungaji bora wa timu hiyo akiwa na mabao 11, sawa na straika mwingine wa timu hiyo Bigirimana Blaise.

Kwa ujumla wao Lusajo na Bigirimana msimu uliopita waliipatia Namungo magoli 22. Na kwa taarifa tu, kwenye mechi tano ilizocheza, Lusajo ameshaifungia KMC mabao mawili, sawa na Bigirimana ambaye naye ameifungia mawili. Hapo takwimu zinaonyesha kuwa magoli yote mawili ya Namungo mpaka sasa yamefungwa na Bigirimana tu. Inawezekana kabisa kuwa Lusajo angekuwapo angeweza kumsaidia mwenzake na hayo mawili ya Lusajo kwa KMC yangeweza kuwa ya Namungo.

Na ingekuwa hivyo, sidhani kama timu hiyo ingekuwa hapo ilipo, au kuonekana kudorora kiasi hiki. Ni kweli Namungo ilihitaji kufanya usajili. Lakini ilitakiwa ihakikishe inawabakisha wachezaji wote muhimu ambao waliipa mafanikio msimu uliopita na si kuwaacha wakiondoka klabuni na kwenda kutafuta wengine ambao hawana uhakika nao.

Namungo ingefuata nyayo za Simba ambayo ilichofanya kwanza ni kubakisha kikosi chake cha msimu uliopita kwa wachezaji wale tegemeo, halafu ikaongeza wengine ambao wameonekana kuingia kwenye kikosi cha kwanza taratibu na si kubadili nusu ya kikosi kizima kwa mara moja.

Kwa sasa si Tanzania tu au Afrika, bali ni dunia nzima, mastraika wenye uwezo wa kufunga mabao wamekuwa adimu sana, hivyo bahati waliokuwa nayo kwa kuwa na Lusajo wasingeitupa kwani ili timu ishinde inahitaji kufunga magoli mengi zaidi ya mpinzani wake.

Kama timu haina mastraika wenye uchu wa kufunga, au kutegemea mmoja tu, ni hatari kwani timu inaweza kufungwa goli moja tu na ikalala.

Mpira wa miguu ni magoli, kwa hiyo ni lazima timu kama Namungo yenye uwezo angalau kidogo wa kipesa, lakini pia inaiwakilisha nchi kwenye mechi za kimataifa, ilitakiwa iwe na mastraika aina ya kina Lusajo ili kufanya vema.

Ndiyo maana hata kocha wa Namungo alipowasili kutoka kwao Rwanda kipindi kile cha usajili na kukuta ameshasajiliwa na KMC, alionyesha kusikitika kuondoka kwa straika huyo. Na akaweka wazi kuondoka kwa Lusajo ni kama vile magoli yameondoka.

Na mimi nashikilia hapo hapo kuwa pamoja na mambo mengine, lakini moja ya mapungufu makubwa ya Namungo msimu huu ni kutokuwa na straika kama Lusajo ili kumsaidia Bigirimana. Ilikuwa ni makosa makubwa kumucha Lusajo aondoke wakati timu ilikuwa na uwezo wa kumzuia.

# Kisarawe yatenga mil. 7/- kununulia taulo za kike

**Na Christina Mwakangale**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani imetenga kiasi cha Sh. milioni saba kwa ajili ya kuwanunulia watoto taulo za kike.

Hayo yalielezwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Jokate Mwegelo, kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, yaliyofanyika Shule ya Sekondari Minaki na kuongoza matembezi ya hisani katika kampeni ya Namthamini, yaliyolenga kukusanya taulo za kike na vifaa vya elimu kwa wasichana.

Matembezi hayo yalianzia ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kisarawe hadi Shule ya Sekondari Minaki yaliandaliwa na kituo cha televisheni na redio ya East Africa kwa kushirikiana na ofisi hiyo, yalihudhuriwa na wadau mbalimbali ikiwamo wanafunzi wa shule za wilayani humo.

Alisema wilaya hiyo inafanya jitihada mbalimbali kuinua elimu ya mtoto wa kike, ikiwamo za kutenga fedha ili kuwanunulia taulo za kike na kujenga shule ya sekondari za bweni kwa wanafunzi wa kike.


Jokate alisema mwaka jana halmashauri ilitenga Sh. milioni nne na imetenga Sh. milioni tatu mwaka huu, ikiwa ni jitihada za kumkwamua mtoto wa kike, huku zikiungwa mkono na EATV East Africa Redio, kupitia kampeni ya Namthamini.

Awali akifungua maadhimisho hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mussa Gama, alisema kuwa wilaya hiyo bado inakabiliwa na tatizo la mimba za utoto ambapo hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kudhibiti hali hiyo.

Meneja Rasilimali Fedha wa kampuni ya The Guardian Limited, Samuel Mtui, alikabidhi taulo za kike, ikiwa ni kuchangia na kutatua changamoto zinazowakwamisha watoto hao kwenye elimu.

Pia Mkuu wa Rasilimali Watu wa kituo cha televisheni ITV na Redio One, Hellen Elipokea, alikabidhi taulo hizo kwa Mkuu wa Masoko na Mauzo wa East Tv na redio, Roy Ronald.

Maadhimisho hayo yaliyoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kisarawe kwa kushirikiana na EATV, yamefanikiwa kupatikana kwa taulo za kike zinazokidhi mahitaji ya wanafunzi wa kike 300 kwa mwaka mzima, pamoja na vifaa vingine vya shule.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Anamringi Macha (mwenye miwani) akipokea msaada wa vitanda na magodoro kutoka kwa Ofisa Mkuu Raslimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonay, wilayani humo juzi, kwa ajili ya kusaidia Hospitali ya Wilaya ya Ushetu, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 20 wapata mimba Msalala ndani ya miezi mitatu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI 20 Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamepata ujauzito kwa kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu na kushindwa kuendelea na masomo.

Kutokana na hali hiyo, wahusika wanalisaidia Jeshi la Ppolisi kuwabaini waliowapa ujauzito.

Ili kutokomeza tatizo hilo, halmashauri hiyo imejipanga kujenga mabweni zaidi katika shule za sekondari, na mpaka sasa wana mabweni sita ambayo yanatumiwa na wanafunzi, huku wakitarajia kujenga pia katika Shule ya Sekondari Buswangili kwa kushirikiana na Mgodi wa Bulyanhulu.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Neema Katengesya, wakati wa mkutano wa waandishi wa habari kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani iliyofanyika jana katika viwanja vya Shule ya Msingi Segese.

Alisema wanafunzi wa kike 20 wa shule za msingi na sekondari wamepata ujauzito na kusitisha masomo, hali ambayo imesababisha kutotimiza malengo yao ya kielimu.

"Halmashauri yetu imezungukwa na wachimbaji wadogo na kusababisha uwapo wa vishawishi vingi kwa wanafunzi wetu wa kike...ili kukabiliana na hali hii, tumeanza kujenga mabweni sita katika shule zetu za sekondari, na hivi karibu tutajenga mbweni Sekondari ya Buswangili kwa kushirikiana na Mgodi wa Bulyanhuru," alisema Katengesya.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri hiyo, Asnath Remtulla, alisema wamekuwa wakiwachukulia hatua za kisheria wamiliki wa migodi midogo ya madini ambayo wamekuwa wakiwatumikisha watoto wagodo wenye umri wa kwenda shule katika shughuli za uchimbaji wa madini na usombaji wa mawe ya dhahabu.

Aidha, alisema wamekuwa wakiwatumia wazee wa kimila katika utoaji wa elimu kwa jamii kuondokana na dhana ya kuwaogesha dawa za mvuto wa mapenzi kwa mabinti zao kwa imani ya kutaka waolewa haraka.

Mratibu wa huduma za simu kwa watoto Tanzania (116), Michael Marwa, alisema, ugumu wa maisha katika familia umesababisha wanafunzi wengi wa kike kujihusisha na vitendo vya mapenzi na wengi kukatisha masomo na kwenda kufanyakazi za ndani.

Pia alisema kuwa, wanaokwenda kufanyakazi za ndani ni wale ambao wako mbioni kuingia darasa la saba na wale ambao wanakwenda kuhitimu elimu ya msingi, na kwamba tatizo hilo limekuwa likisababisha uwapo wa watoto wengi wa kike wasiokuwa na elimu.

# Mgombea ajitwisha zigo migogoro sugu ya ardhi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MGOMBEA ubunge wa Dodoma Mjini kwa tiketi ya CHADEMA, Aisha Madoga, amesema endapo akichaguliwa, atahakikisha anatatua kero ya ardhi ambayo imekuwa sugu kwa muda mrefu.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa kampeni Kata ya Uhuru, Madoga alisema akichaguliwa atasimamia suala la ardhi ambapo hivi sasa imekuwa kero kutokana na kwenye mabaraza ya kata na mahakama mbalimbali kuwa na kesi nyingi zisizotatulika.

"Msifanye makosa kwa kuchagua viongozi ambao wanafanya kazi zao kwa mazoea bila kujali kero zilizopo, mkafanye chaguo lililo sahihi na msichague kutokana na mvuto wa kuyaona mabango na madudu ya kijani ambayo yamewazunguka," alisema.

Aliwaomba wananchi kumchagua ili awaletee maendeleo na kuacha kuchagua kwa itikadi ya mazoea ambayo yamekuwa hayatatui kero isipokuwa kujinadi kwa mbwembwe wakiwa majukwaani.

Alisema wakazi wa Dodoma kwa miaka mingi hiyo wamekuwa wakikumbana na migogoro hiyo kutokana na usimamizi mbovu, na kuwaomba kufanya mabadiliko kwa kuchagua chama ambacho kitahakikisha kinaondoa adha hiyo.

"Mkituchagua mimi na diwani wa Kata ya Uhuru wa CHADEMA, tutaenda kusimamia kodi ya ardhi ya kila mwanaDodoma ili kupata haki yake ya umiliki kwa uhuru na haki pamoja na urasilimishaji wa ardhi," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Uhuru, Salma Mambo, aliwaomba wakazi wa mtaa huo kumchagua ili arudishe eneo la kiwanja cha kuchezea mpira cha Shule ya Msingi ya Uhuru, ambacho Jiji limeamua kukifanya kuwa stendi ya malori ya mizigo.

# Hatimaye mlinzi wa bilionea Laizer azikwa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

HATIMAYE mwili wa Manase William (47), mlinzi wa bilionea wa madini ya Tanzanite, Saniniu Laizer, aliyeuawa kinyama mgodini Mererani, umezikwa jana nyumbani kwake Ilkiding'a, wilayani Arumeru huku familia ikitishia kuvunja chungu ili kukomesha mauaji ya namna hiyo yanayotokea katika machimbo hayo.

Kabla ya mazishi hayo upande wa familia uliingia kwenye mgogoro mkubwa na upande wa mmiliki wa mgodi, Laizer kuhusu kifo hicho huku Meneja wa Mgodi, Kiria Laizer na mdhamini wa mgodi, George Nditika, kufukuzwa kwenye kikao cha familia ya marehemu. Akizungumza katika mazishi hayo yaliyohudhuriwa na umati mkubwa wa waombolezaji bila kuwapo upande wa wamiliki wa mgodi, kaka mkubwa wa marehemu, Peter William, aliitaka Jeshi la Polisi, mkoani Manyara kuharakisha uchunguzi ili kubaini vinara wa tukio hilo na kuchukuliwa hatua.

Hata hivyo, alisema familia haitakaa kimya kwa kuwa wanaamini ndugu yao alikatishwa uhai na watu wasiojulikana, kwa kutumia mila zao wanatafakari kuvunja chungu kama sehemu ya kuwaibua wahalifu na kukomesha matukio ya namna hiyo.

Kwa mujibu wa jamii hiyo ya Kimasai kitendo cha kuvunja chungu ni jambo ambalo wanaamini litamwonyesha aliyehusika na tukio hilo akiwa hai ama amekufa.

Mchungaji wa Kanisa la KKKT, Zacharia Mollel, aliyeongoza maziko hayo, aliitaka familia hiyo kutafakari kwa kina jambo hilo na kumwachia Mungu kwa kuwa kwake hakuna masuala ya kuvunja chungu.

"Tusitafute kulipiza kisasi kwa njia isiyo sawa, tunatumaini Mungu ndiye mwenye uwezo wa kulipa kisasi, tusikimbilie kuvunja chungu, Wakristo hawavunji chungu," alisema Mchungaji Mollel. Alisema kuwa hakuna ubishi kuwa Manase aliuawa, lakini kwa kuwa jambo hilo lipo kwenye vyombo vya sheria viachwe vifanye kazi yake.

Akizungumzia tukio la kutofika katika mazishi ya marehemu mlinzi wake, Lazier alisema upande marehemu hawakutaka ushirikiano.

"Kama ndugu zangu walifukuzwa kwenye kikao cha familia ya marehemu sasa mimi nitawezaje kwenda tunachofanya ni kuingalia utaratibu utakaofaa kumsaidia mke wa marehemu," alisema Laizer.

Marehemu Manase anadaiwa kuuawa na watu wasiojulika akiwa kazini Septemba 27, mwaka huu na mwili wake kukutwa umeegeshwa pembezoni kwa mgodi. Hadi sasa watu saba wakiwamo wafanyakazi wa bilionea Laizer wanashikiliwa na polisi mkoani Manyara.

# AMCOs zadaiwa mil. 5.2/- za vipimo

**Na Said Hamdani,** LINDI

OFISI ya Wakala wa Vipimo Mkoa wa Lindi, inadai Sh. milioni 5.2 katika vyama 23 vya msingi na ushirika (AMCO's), ambazo ni malipo ya ada kwa kazi iliyofanywa ya kuhakiki na kurekebisha mizani zilizobainika kuwa na tatizo kwa msimu wa ununuzi wakorosho na ufuta 2019/2020.

Meneja wa Wakala wa Vipimo mkoani humo, Andrew Mbwambo, aliyaeleza hayo katika mahojiano maalumu na Nipashe.

Alisema malipo hayo yanatokana na kazi iliyofanyika ya kuhakiki mizani zinazotumika kupima mazao kama vile ufuta na korosho kabla ya msimu kuanza mwaka 2019/2020.

Mbwambo alisema katika kipindi hicho cha msimu vyama 112 vya msingi vilivyofanyiwa uhakiki na marekebisho ya mizani ni 23 bado havijakamilisha kulipa ada zao, licha ya kukumbushwa kufanya hivyo mara kwa mara.

"Hizi Amcos 23 ndizo hazijakamilisha malipo ya ada za uhakiki wa mizani zake, licha ya kukumbushwa mara kwa mara," alisema Mbwambo.

Aidha, alivitaja vyama hivyo vya msingi na ushirika vinavyodaiwa na idadi yake kwa kila Wilaya kwenye mabano Ruangwa (9), Nachingwea (8) Liwale (4) na Kilwa (2).

Kwa mujibu wa meneja huyo, mizani zinapokuwa sahihi hupunguza na kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi wanaopata huduma za kupimiwa bidhaa, pamoja na kuimarisha uchumi na mapato ya serikali kwa ujumla.

Aidha, aliwataka viongozi wa vyama hivyo husika vinavyodaiwa kuhakikisha wanalipa madeni ya ada husika kuepuka kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo, ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani kudai malipo hayo.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu (mwenye miwani), akikabidhi moja ya vyerehani kwa wanafunzi vinara wa dawati la ukatili dhidi ya watoto Shule ya Sekondari Dundani, wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani jana. Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Shirika la HakiElimu, Dk. John Kalage.
**PICHA: ZUWENA SHAME**

# Wanafunzi waelimishwa sababu wazee kuwa na macho mekundu

**Na Neema Sakawa,** KAHAMA

WANAFUNZI wa shule za msingi katika Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wametakiwa kusaidia kutoa elimu kwa wazazi kuhusu fikra potofu ya kuwa wazee wenye macho mekundu wanajishughulisha na kazi za uchawi.

Msaidizi wa Daktari wa Mifugo kutoka katika Shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na Ustawi wa Wanyama nchini (TAPO), Abdul Kalegi, alisema hayo wakati akitoa elimu hiyo kwa wanafunzi hao pamoja na matumizi sahihi ya mnyama punda katika jamii.

Alisema hali hiyo ya kuwa na macho mekundu inatokana na uhaba wa nishati ya kuni katika maeneo yao hali ambayo iyowafanya kutumia nishati ya kinyesi cha ng'ombe kilichokauka kupikia chakula wakati wote.

Kalegi alisema matumizi ya kinyesi cha ng'ombe kama nishati katika kupikia ni ya kurithi kutoka kwa mababu zao ambao walikuwa wakifanya hivyo kuni zinapokuwa adimu katika maeneo yao.

Dk. Kalegi pia, aliwataka wanafunzi hao kutoa elimu kwa wazazi wao kuhusu kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti katika maeneo husika kuwasaidia kutumia miti hiyo kama kuni ambazo zitapunguza watu kuwa na macho mekundu kwa sababu ya kutumia kinyesi cha ng'ombe.

Shirika la TAPO linatoa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi ikiwa ni pamoja na kupanda miti ili kuondoa hali hiyo maeneo ya shule, nyumbani na kuwake mazingira katika hali bora.

Vile vile, shirika hilo lilitoa elimu ya matumizi ya punda kwa wanafunzi wa darasa la nne kuacha tabia ya kuwafanyisha kazi kwa muda mwingi na unyanyasaji kwa wanyama hao ambao ni msaada mkubwa katika jamii kwa kuwaongezea kipato.

"Punda ni mnyama mpole sana na akimtumia vizuri anaweza kukuza uchumi katika familia kwa kuwaingizia kipato kwa kubeba mizigo," alisema.

Pia, shirika hilo lilitoa elimu ya kujua magonjwa anayopata punda na jinsi ya kumkinga na kuwatibu waliokuwa tayari wameathirika.

# Wanaopakana Hifadhi ya Ruaha wataka elimu

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa MBEYA**

WAKAZI wanaoishi katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha Kanda ya Kusini, wameomba kupatiwa elimu zaidi kuhusiana na masuala ya uhifadhi na wanyamapori, ili kumaliza migogoro kati ya wananchi na hifadhi.

Wameeleza kuwa elimu waliyonayo ni ndogo na baadhi ya wanavijiji hawana kabisa, jambo ambalo linasababisha kushindwa kutatua changamoto zinazohusiana na wanyamapori na uhifadhi.

Waliyasema hayo wakati wakihojiwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) katika ziara iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Akizungumza kwa niaba yao, Ofisa Mtendaji wa Kitongoji cha Mawindi, Edson Kilemile, alisema licha ya kuwapo na faida za kuwa karibu na hifadhi, bado wanachangamoto nyingi ikiwamo elimu haba katika uhifadhi wa wanyamapori.

Alisema kukosekana kwa elimu kumesababisha kuwapo na migogoro isiyo ya lazima.

Alisema baadhi ya wananchi wamejikuta wakiwakimbia watu wa sekta ya uhifadhi kutokana na mtazamo hasi waliokuwa nao, licha ya kwamba hawajafanya uhalifu wowote.

Naye Kamishna Msaidizi wa Hifadhi Kanda ya Kusini, Pius Mzimbe, alisema wana kitengo maalum cha ujirani mwema moja ya majukumu yake ni kutoa elimu ya masuala ya uhifadhi wa wanyamapori na kuimarisha uhusiano kati ya wana vijiji wanaozunguka hifadhi.

Alisema ofisi yake ina mikakati ya kuongeza nguvu kwenye elimu kwa wananchi, ili kuimarisha ushirikiano uliokuwapo.Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema baadhi ya wana vijiji wamekuwa wakitumia suala la elimu kama kisingizio cha kujilinda.

Alisema halmashauri kwa kushirikana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) walifanikiwa kupeleka wataalamu wanaohusiana na masuala mbalimbali ya sekta hiyo na kutoa elimu kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi.




Mafundi wa kampuni ya ujenzi China Railway Seventh Group (CRSG), wakiweka matuta katika eneo la Shule ya Mama Salma Kikwete, eneo la Kijitonyama, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ili kuyafanya magari yapunguze mwendo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# PM ahamasisha uwekezaji sekta ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Mjaliwa, ameitaka Kampuni ya mbolea ya YARA kuongeza uwekezaji wa mbolea nchini sambamba na kuinua sekta ya kilimo ili kuongeza tija na manufaa zaidi kwa mkulima.

Akizungumza baada ya kutembelea makao makuu ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam juzi pamoja mambo mengine, Majaliwa alipongeza uwekezaji uliofanywa na kampuni hiyo sambamba na kutaka uwekezaji zaidi kwenye sekta ya kilimo ambayo inaajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania.

"Serikali imeweka kipaumbele kwenye sekta ya kilimo ili kuwa na uhakika wa malighafi viwandani na kufanikisha azma yake ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Tunawapongeza YARA na wadau wengine kwa namna wanavyounga mkono juhudi hizi za serikali," alisema.

Alifurahishwa na juhudi za kampuni hiyo kuwasaidia wakulima wadogo nchini katika kupunguza tatizo la ajira, kuinua sekta ya kilimo na kuhakikisha usalama wa chakula unakuwapo pamoja na kuchangia pato la Taifa.

Aidha, aliwahakikishia wawekezaji nchini kuwa serikali itaendelea kutatua changamoto zilizopo katika uwekezaji ili kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta mbalimbali za uchumi.

"Tumeona namna YARA mnavyofanya kazi zenu katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Tabora, Njombe na Kilimanjaro. Serikali itaendelea kushirikiana nanyi kwa kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kuwafikia wakulima wengi zaidi," alisema.

Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, alisema nchi yake imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono maendeleo ya sekta ya kilimo barani Afrika ikiwamo Tanzania.

"Afrika imekuwa na changamoto ya upatikanaji wa chakula, YARA imekuwa na mipango mingi katika kuhakikisha panakuwapo na usalama wa chakula.

Naye Mkrugenzi Mtendaji wa YARA Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema kampuni yake itaendelea kusimamia ubora wa mbolea ili kuongeza uzalishaji wa mazao hapa nchini sambamba na kutengeneza ajira kwa Watanzania.

"Tutaendelea kutengeneza mbolea bora ili kuzidi kumnufaisha mkulima, lakini kuzidi kutoa ajira ambapo mpaka sasa tumetengeneza ajira rasmi zaidi ya 60 na ajira zisizo za kudumu zaidi ya 300," alisema Odhiambo.

# Kiwanda cha pamba Kahama chafufuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amezindua kiwanda cha pamba cha Kahama (KACU) kilichofufuliwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ambapo zaidi ya shilingi bilioni 4.6 zimeshatolewa.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Bashe alisema kufufuliwa kwa kiwanda hicho ni dhamira ya kweli ya serikali ya kuinua na kuongeza uzalisha wa mazao yote ya kimkakati ikiwamo pamba nchini.

"Kuzinduliwa kwa kiwanda hiki inamaana kubwa sana kwa wakulima wa pamba kwa maeneo hayo kwani kitasaidia kuongeza uzalishaji wa pamba na kuwaongezea kipato wakulima wa zao hili,'' alisema.

Alisema kutokana na umuhimu wa kiwanda hicho, alilazimika kuhamishia ofisi yake TADB, ili kuhakikisha zoezi la kukifufua kiwanda linakamilika kwa wakati na kuleta mapinduzi ya dhahabu nyeupe (pamba).

"Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza benki ya TADB na benki washirika wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mrajisi wa Ushirika na wengine kwa namna mlivyosimamia kukamilika kwa zoezi la kufufua kiwanda hiki ambacho kitawanufaisha wakulima mkoani Shinyanga,'' alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema uzinduzi wa kiwanda hicho utaongeza tija kwa wakulima kwa kuwa bei ya pamba itaongezeka na kuwafanya wamudu gharama za maisha na kuchangia ukuaji wa pato la Taifa.

"Uzinduzi wa kiwanda hiki utaongeza uzalishaji wa pamba ambayo ni malighafi muhimu kwa viwanda vya ndani, lakini thamani ya zao la pamba litaongezeka na kuzidi kutoa mchango wake katika ukuaji wa pato la Taifa na mkulima mmoja mmoja," alisema Justine.

# RC ataka wazawa kupewa kipaumbele

**Na Tiganya Vincent**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameagiza Watanzania wapewe kipaumbele wakati wa utoaji wa kazi zote ndogo ambazo hazihitaji ujuzi kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara yake ya kukagua mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kuleta mkoani Tabora na uboreshaji wa bomba la maji kutoka katika Bwawa la Igombe kwa ajili ya wakazi wa Manispaa ya Tabora.

Dk. Sengati alisema maelekezo ya serikali yanataka kazi ambazo hazihitaji ujuzi wa hali ya juu kwenye miradi mikubwa ukiwamo wa ujenzi wa bomba la maji kutoka Ziwa Victoria na ile ya barabara wapewe Watanzania na sio wageni.

Aliongeza kuwa hata pale ambapo kutakuwa na uhitaji wa kutumia mafundi wa nje ya Tanzania, ni lazima wafanye Watanzania ili nao wapate ujuzi huo na pindi wataalamu wa kigeni watakapoondoka waweze kuendeleza ujuzi huo kwa manufaa ya nchi.

Mhandisi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA), Athuman Kiludumya, alisema kwenye mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria wanaotakiwa kufanyakazi kutoka nje ya nchi ni wataalamu wa juu na sio wa kufanyakazi ndogo kama wa kuchomelea.

# Kikosi maalum kukabiliana na wanyamapori waharibifu

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, ameagiza kuundwa kwa kikosi maalum cha kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu ili kuokoa mali na maisha ya binadamu.

Aidha, ameagiza kuhakikisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za wanyamapori wakali na waharibifu ukamilishwe kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2020/21.

Dk. Kigwangalla alitoa maagizo hayo jana wakati wa uzinduzi wa mkakati wa kitaifa wa kusimamia utatuzi wa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori wa mwaka 2020 hadi 2024 uliofanyika jijini hapa.

Alisema kikosi hicho kitakuwa chini ya Mfumo wa Jeshi la Uhifadhi ili kukabiliana na matukio kwa ajili ya kuokoa maisha na mali za binadamu dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Pia, aliagiza kuwa utaratibu wa kutenga maeneo ya shoroba na mtawanyiko wa wanyamapori uharakishwe ili kudhibiti mwingiliano wa njia za wanyama.

"Kwa Taasisi za Wizara yetu TANAPA, NCAA, TAWA na TFS naelekeza mtenge bajeti katika kutekeleza mkakati huu," alisema.

Aliziomba Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kupunguza migogoro.

Aliongeza kuwa wizara hiyo itashirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuweka suala la migogoro kati ya binadamu na wanyamapori katika mitaala ili lifundishwe kuanzia shule za awali, msingi na sekondari.

Naye Mkurungenzi wa Idara ya Wanyamapori, Dk. Maurius Msuha, alisema lengo la mkakati huo ni kupunguza migogoro iliyokuwapo kwa baadhi ya watu wanaoishi jirani na hifadhi za taifa.

Alisema malengo mengine ni kuwezesha jamii kutumia njia sahihi zinazofaa kupunguza madhara yanayosababishwa na wanyamapori.

Aliyataja baadhi ya madhara hayo kuwa ni kama vifo vya watu, majeruhi, uharibifu wa mazao, mifugo na mali zingine.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Aloyce Nzuki, alisema pamoja na kuzinduliwa kwa mpango huo watandelea na kutoa elimu kwa wananchi namna ya kujikinga na madhara ya wanyamapori hao.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko, Mawasiliano na Uraia katika benki ya NCBA Tanzania, Caroline Mbaga (katikati), akitoa mada wakati wa Jukwaa la Wanawake katika sekta ya fedha, lililowashirikisha wadau wanawake kutoka sekta za kibenki na bima, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, na kudhaminiwa na benki hiyo. Kulia ni Meneja Mkuu wa Usimamizi wa Takwimu na Uhatarishi wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Annet Magogo na Ofisa Mkuu Mtendaji wa AAR Insurance, Violet Mardichai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Katambi aahidi fursa wafugaji na wakulima

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini kupitia CCM, Patrobas Katambi, amemwaga sera zake kwa wananchi wa jimbo hilo, na kuahidi kuwa endapo wakimchangua, atahakikisha anakuza uchumi wa wafugaji na wakulima.

Katambi alitoa ahadi hizo juzi kwenye eneo la soko kuu mjini Shinyanga, wakati akinadi sera zake kwa wananchi wa jimbo hilo, ili siku ya uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu wampigie kura za ushindi na kuwa mbunge wao.

Alisema kwa mujibu wa utafiti, Jimbo la Shinyanga mjini halina wafugaji wa kutosha, ambao wataweza kuhudumia kiwanda cha nyama pamoja na machinjio ya kisasa, na kuahidi wananchi kuwa endapo wakimchagua, atatenga eneo kubwa kwa ajili ya kufugia mifugo tu na kuinua uchumi wa mfugaji.

"Mimi nataka kiwanda hiki cha nyama ambacho tutakifufua, pamoja na machinjio ya kisasa iliyopo, malighafi yake ambayo ni ng'ombe itoke kwa wazawa ambao ni wana-Shinyanga wenyewe ili muinuke kiuchumi," alisema Katambi.

Pia alisema kwa upande wa kilimo, ataleta Taasisi ya Utafiti ya Kilimo (TARI), kubaini mbegu za kilimo ambazo zinakubalika kwenye ardhi ya Shinyanga, ili wananchi walime kilimo chenye tija ambacho kitawainua kiuchumi, badala yakufanya kilimo cha kubahatisha.

Katika hatua nyingine, aliahidi kuboresha mazingira ya wafanyabiashara, ikiwamo kulikarabati soko kuu la mjini Shinyanga, kuleta wawekezaji, pamoja na wafanyabiashara wa usafirishaji wa baiskeli, daladala, bodaboda, na bajaji na kuwapatia mikopo kupitia vikundi ili wapate kupanuka kibiashara.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, aliwataka wakazi wa Jimbo la Shinyanga Mjini siku ya kupiga kura wasifanye makosa bali wamchangue Katambi, pamoja na mgombea urais, John Magufuli, ili wawaletee maendeleo na Shinyanga iendane na uchumi wa kati.

## Mgombea ACT: Wananchi wawachague watatua kero

**Na Christina Mwakangale**

MGOMBEA udiwani Kata ya Masiwani jijini Tanga, kupitia ACT-Wazalendo, Jumanne Iddi Selemani, amesema wananchi wasichague 'digrii' (shahada) badala yake wamchague mtatua kero zao.

Alitoa kauli hiyo jijini Tanga hivi karibuni wakati akizungumza na Nipashe kueleza namna atakavyotatua kero za wananchi wa eneo hilo, na kufafanua kuwa nafasi ya udiwani ni muhimu kwa kuwa husimamia shughuli za maendeleo kuanzia ngazi ya chini kwenye jamii.

Alisema wananchi wawachague wagombea wanaofahamu changamoto za kata husika, hivyo kuwa rahisi kuzitatua, na kwamba yeye ndiye anafaa.

"Mwaka 2014 nilichaguliwa kuwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa wa Mbugani, nilifanikisha kuwapo kwa huduma ya maji, umeme, madaraja, barabara na hadi mwaka 2019 vikakamilika," alisema Jumanne na kuongeza:

Nilifanikisha kupatikana pia kwa usafiri wa umma eneo la kutoka Tanga mjini hadi Masiwani Mbugani ambako kulikuwa na miundombinu duni, kipindi hicho."

Alisema iwapo akichaguliwa atasimamia kukamilika ujenzi wa miundombinu na barabara kwa kipindi cha miaka mitano.

"Kama ambavyo niliweza kuongoza kwenye mtaa hapo nyuma na katika udiwani nitaweza," alisema.

"Tunavyokwenda katika nafasi hizi udiwani, ni zetu sisi wananchi wa kawaida hususan maendeleo, tukienda kuchagua viongozi tuchague wanaofahamu mazingira ya eneo au kata husika."

## Wazazi, walezi wapewa angalizo kesi za ukatili

**Na Yasmine Protace**

WAZAZI na walezi wametakiwa kutomalizana majumbani na watuhumiwa wanaodaiwa kufanya vitendo vya ukatili kwa watoto wao, badala yake kutoa taarifa ili hatua dhidi yao zichukuliwe.

Pia imeelezwa kuwa vitisho ambavyo vinatolewa na watuhumiwa kwa wazazi na walezi ambao watoto wao wamefanyiwa ukatili, vimesababisha hata kesi kuchelewa kufikishwa mahakamani.

Hayo yalisemwa na Naibu Msajili katika Mahakama Kuu, Nyegulila Mwaseba, katika semina za Jinsia na Maendeleo ya Jamii (GDSS) zinazoratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

"Matukio ya ukatili yapo, watoto wanafanyiwa ukatili, lakini familia zao zinaogopa kusema kutokana na vitisho wanavyovipata kutoka kwa watuhumiwa," alisema.

Alisema kesi zinapofikishwa mahakamani hafiki kwa wakati na hata wakati mwingine wanaofanyiwa ukatili wanapopelekwa wanakuwa wameshaharibika hata sehemu za siri kutokana na kukaa muda mrefu bila kutoa taarifa ili hatua zichukuliwe kwa wahusika.

Alisema kinachosikitisha ni pale mtoto anapofanyiwa ukatili halafu hafikishwi kwa wakati sehemu husika ili asaidiwe kisheria pamoja na kukaa kimya kunachangia watoto kuharibika miili yao.

Alisema watoto wanayohaki ya kulindwa na kama wamefanyiwa ukatili ni jukumu la wazazi au walezi kuwapeleka polisi ili wasimamiwe kisheria.


NIPASHE JUMATATU OKTOBA 12, 2020

Nipashe

Spotika



10 - BORA YA NAMBA SABA WA WAKATI WOTE DUNIANII UK. 12&13



Jack Wilshere

# NYOTA WA5 AMBAO DIRISHA EPL KWAO BADO LIPO WAZI

**LONDON, England**

DIRISHA la usajili lilifungwa Oktoba 5, mwaka huu na sasa klabu zitatulia na vikosi vyao vipya baada ya uvumi wa miezi kadhaa.

Hata hivyo, timu za Ligi Kuu ya England bado zina uwezo wa kuimarisha vikosi vyao kwa kwenda kwenye soka la wachezaji waliopo huru, yaani wale waliomaliza mikataba na timu zao za zamani.

Tayari baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa ambao wapo huru wameshasajiliwa na timu kadhaa.

Manchester United imemsajili Edinson Cavani kwa uhamisho huru siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la usajili.

Cavani alibaki kuwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake kule kwenye klabu ya PSG ya Ufaransa.

Hata hivyo, bado kuna majina makubwa yanayotambulika ambayo yanaweza kusajiliwa kwa kipindi hiki.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wapo huru na klabu za Ligi Kuu ya England zinaweza kuwasajili ili kuimarisha vikosi vyao, shuka nayo...

**#5. Nathaniel Clyne**

Mkataba wa Nathaniel Clyne na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya England, Liverpool ulimalizika kipindi cha majira ya joto na kwa sasa yupo huru. Mlinzi huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 29, ambaye alianza maisha ya soka kule Crystal Palace, kwa sasa anafanya nao mazoezi na imeripotiwa kuwa yupo tayari kuhamia hapo kwenye dimba la Selhurst Park.

**#4. Shinji Kagawa**

Kiungo wa zamani wa Manchester United, Shinji Kagawa kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuvunja mkataba wake na Real Zaragoza ya Hispania. Real Zaragoza ilitangaza kuvunja mkataba na mchezaji huyo katika taarifa iliyosomeka, "Real Zaragoza imemaliza mkataba kwa maelewano na mchezaji Shinji Kagawa."

Kagawa ana umri wa miaka 31 na ana uzoefu wa kucheza katika soka la Uingereza na Ujerumani.

**#3. Alexandre Pato na Daniel Sturridge**

Alexandre Pato alivunja mkataba wake na Sao Paulo Agosti mwaka huu na kwa sasa ni mchezaji huru na anaweza kusajiliwa popote.

Internacional imeripotiwa kuwania kumsajili straika huyo mwenye umri wa miaka 31, lakini raia huyo wa Brazil anaonekana hataki kucheza tena nyumbani.

Pato kamwe hakuweza kuthibitisha ubora wake wakati wa ujana wakati akicheza kwa muda mrefu kule AC Milan kuanzia mwaka 2007 hadi 2013. Crystal Palace inatajwa kuwania kumsajili mchezaji huyo ili kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.

Wakati huo huo, straika wa zamani wa Liverpool, Daniel Sturridge pia ni mchezaji huru tangu Machi mwaka huu. Klabu yake ya utotoni ya Aston Villa inatajwa kwamba inataka kumsajili nyota huyo wa zamani wa Liverpool.

**#2. Danny Welbeck**

Danny Welbeck kwa sasa amevunja mkataba wake na Watford kwa maelewano. Welbeck amekaa kwa muda mfupi pale Watford na sasa anataka kwenda sehemu nyingine.

Watford wasingeweza kuendelea kubaki naye kutokana na mshahara wake wa pauni 100,000 kwa wiki. Lakini klabu ya Crystal Palace imeonyesha nia ya kutaka huduma yake.

**#1. Jack Wilshere**

Majeruhi yamekuwa yakimwandama zaidi Muingereza huyu mwenye umri wa miaka 28, na West Ham wakaamua kuvunja mkataba naye, kwani kwa kipindi chote alichokuwa nao amekuwa majeruhi.

Pengine Wilshere angependa kucheza nje ya Ligi Kuu ya England, lakini anaweza kupata nafasi ya kucheza kwenye klabu yoyote itakayomhitaji kwa sasa.

Licha ya kusumbuliwa na majeruhi, lakini nyota huyo anajulikana kwa uwezo wake mkubwa katika dimba la kati hasa wakati akitamba kule Arsenal.

## ISIKUPITE

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, amekiri kuwa bado ni ndoto yake siku moja kuichezea Real Madrid ya Hispania, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, akaongeza "nitafanya kila liwezekanalo kuiweka United sehemu ambayo klabu hii inastahili kuwapo".



## Extra Time



# 10 - BORA YA NAMBA SABA WA WAKATI WOTE DUNIANI

Ronaldo

**LONDON, England**

JEZI namba saba katika mpira wa miguu kawaida huvaliwa na mawinga na washambuliaji wa pili, lakini imepambwa na washambuliaji wengine maarufu walioicheza mchezo huo.

Kiutamaduni, jezi Na. 7 imekuwa na wachezaji wanaopenda kupiga chenga na kukimbilia nyuma ya ulinzi wa wapinzani kupiga mijeledi kuwapelekea wenzao eneo la katikati.

Hata hivyo, kwenye soka la kisasa, majukumu ya mchezaji Na. 7 yamebadilika kutokana na wakati.

Aidha, mchezaji hodari katika timu mara nyingi hupewa heshima ya kuvaa jezi Na. 7. Baadhi ya wachezaji mashuhuri katika mchezo huo, wote wanaocheza sasa na waliostaafu, wamevaa jezi hii kwa timu kwa miaka iliyopita.

Kwenye makala haya, hebu tuangalie wachezaji 10-bora waliowahi kuvaa jezi Na. 7, bila kuangalia mpangilio wao, ambao walikuwa alama ya jezi hiyo, twende sasa...

**# 10. Raul**

Raul Gonzalez wa Real Madrid, anayejulikana zaidi kwa jina lake tu, ni mmoja wa idadi maarufu zaidi ya saba si tu katika historia ya klabu bora, lakini kwenye mchezo wenyewe.

Raul, ambaye alikulia kwenye akademi ya Madrid, alirithi jezi maarufu ya Real Madrid Na.7 kutoka kwa Emilio Butragueno aliyestaafu mwaka 1995, akiwa na miaka 17 na hakuangalia nyuma tena.

Wakati wake wa mafanikio ya miaka mingi pale kwenye dimba la Bernabeu, Raul alifunga mabao mengi, 323 yeye akiwa namba saba wa mwisho kuwa kufungaji bora wa klabu hiyo kabla ya ujio wa Cristiano Ronaldo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alikuwa kwenye kiwango bora katika msimu wa 2000-01 kwani mabao yake 32 kwenye mashindano yote yalisaidia Real Madrid kushinda taji la LaLiga na kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Raul aliondoka kwenda Schalke mnamo mwaka 2010 baada ya kushinda mataji sita ya ligi na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#9. Franck Ribery**

Franck Ribery aliwasili Bayern Munich katika msimu wa joto wa 2007 na kurithi jezi Na. 7 ya klabu hiyo kutoka kwa Mehmet Scholl aliyekuwa amestaafu.

Si kila mtu alikuwa na imani kubwa kwake baada ya kutua pale Bavaria, lakini Ribery aliweza kuthibitisha ubora wake na kuwa kipenzi cha Bayern kwa kufunga bao kwenye mchezo wake wa pili wa Bundesliga, na hakutaka kuangalia tena nyuma kutoka hapo.

Alifunga mabao 11 na kusaidia nane wakati Bayern wakishinda taji la ligi na akawa mchezaji wa pili mgeni ambaye si raia wa Ujerumani kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka.

Mwaka mmoja baadaye, Ribery aliungana na Arjen Robben, na wawili hao walipewa jina la utani la 'Robbery' na wakatawala safu zote za winga, Ribery akicheza kushoto na Robben kulia. Mawinga hao walifanya Bayern kutawala soka la Ujerumani.

Kwa kipindi cha misimu 12 aliyokaa pale Bavaria, Ribery licha ya kukumbwa na majeraha ya mara kwa mara, alifanikiwa kufunga mabao 124 na kutoa pasi za mwisho 182 na akaipiku rekodi ya Hasan Salihamidzic na kuwa mchezaji wa kigeni aliyecheza mechi nyingi zaidi.

Ribery aliyemaliza kipindi cha kucheza Bayern akiwa na mataji 23, msimu uliopita alisajiliwa kuichezea Fiorentina.

**#8. Kevin Keegan**

Kevin Keegan ni mmoja wa wachezaji wa aina yake katika historia ya Liverpool.

Kwa kipindi cha misimu sita aliyocheza pale Anfield kutoka mwaka 1971 hadi 1977, Keegan alikuwa alama ya Na. 7.

Keegan alifunga mabao 90 na kutoa pasi za mwisho 56 katika mashindano yote, huku akishinda taji la ligi mara tatu, la Ulaya moja na lile la FA.

**#7. David Beckham**

David Beckham, alijulikana kwa uwezo wake wa kupiga pasi kutoka winga ya kulia hasa kwa mipira iliyokufa, alikuwa namba saba aliyeutendea haki mchezo wa soka kwenye historia yake.

Beckham kwa mara ya kwanza alipewa jezi namba saba akiwa na umri wa miaka 21 pale Manchester United baada ya awali kuvaliwa na Eric Cantona, aliyeondoka klabuni hapo.

Muingereza huyo, ambaye hakuvaa jezi Na. 7 katika kipindi chake cha miaka minne ya kucheza kule Real Madrid, alifunga mabao 127 na kutoa pasi za mwisho 202 kwa kipindi alichozichezea klabu sita tofauti.

Beckham alifunga mabao ya adhabu ndogo 65 kwa kipindi cha uchezaji wake wa karibia miongo miwili kwenye ngazi ya klabu na nchi, yakiwamo mabao 29 kwa Manchester United na 14 kwa Real Madrid.

**#6. Eric Cantona**

Eric Cantona alianza kutamba kule Leeds United mwaka 1992 wakati alipofunga mabao tisa na kuwezesha klabu yake hiyo kuipiku Manchester United kushinda taji la Ligi Kuu kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 18.

Baada ya kutokuwa na mahusiano mazuri na kocha wake pale Leeds, Manchester United wakamuita Cantona, na kuanzia hapo akawa na mafanikio makubwa mbele yake.

Kama mengi aliyoyafanya kule kwenye dimba la Elland Road, Cantona akawa kipenzi namba moja cha mashabiki pale Old Trafford.

Mfaransa huyo alifunga mabao 61 na pasi za mwisho 81 katika misimu minne na nusu pale Manchester United, huku akitwaa mataji manne ya Ligi Kuu, matano ya Super na mawili ya FA.

**#5. Luis Figo**

Luis Figo aliitengeneza jezi Na. 7, mwenyewe pale Sporting Lisbon na baadaye FC Barcelona ambako alishinda taji la Ligi Kuu mfululizo pamoja na lile la Hispania.

Figo akawakasirisha mashabiki kwa uamuzi wake wa kuondoka Barcelona na kwenda kwa wapinzani wao wakubwa, Real Madrid. Ingawa nyota huyo wa zamani wa Ureno hakuvaa jezi namba saba pale Madrid, lakini alikuwa na wakati mzuri wa kufunga mabao yake 56 na pasi za mwisho 93.

Baadaye mchezaji huyo aliyecheza mechi nyingi zaidi kwa timu ya Taifa ya Ureno, alihamia Inter Milan ambapo alipewa jezi Na. 7.

**#4. Bastian Schweinsteiger**

Ingawa Bastian Schweinsteiger hajawahi kuvaa jezi namba saba kwa klabu zote alizozichezea, nyota huyo aliitendea haki jezi hiyo akiwa na kikosi cha timu ya Taifa ya Ujerumani hasa wakati wakitwaa Kombe la Dunia mwaka 2014.

Schweinsteiger alivaa jezi Na. 31 wakati akicheza pale Bayern kwa misimu 13, misimu miwili na Manchester United na mitatu na Chicago Bulls kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

**#3. George Best**

George Best ni mmoja wa wachezaji magwiji kwenye historia ya soka na anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kuwahi kuucheza mchezo huo.

Raia huyo wa Ireland Kaskazini alikuwa na wakati bora zaidi akiwa anavaa jezi hiyo katika kipindi chake cha uchezaji pale Manchester United.

Katika kipindi alichocheza pale Man United, Best alishinda mataji mawili ya Ligi, Super, FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#2. Garrincha**

Manuel Francisco dos Santos, maarufu zaidi kama Garrincha, ni mmoja wa wachezaji wanaojua kupiga chenga wa wakati wote.

Winga huyo wa kulia alikuwa na balaa zito kwenye nafasi hiyo kwa kutupia krosi zenye macho. Kwa kipindi ambacho alikosekana Pele, Garrincha ndiye alikuwa mchezaji muhimu wa Brazil wakati Brazil wakitetea Kombe la Dunia mwaka 1962, ambapo pia aliibuka mfungaji bora wa mashindano hayo na kushinda Kiatu cha Dhahabu.

Garrincha kwa kipindi chote cha uchezaji aliitumikia zaidi timu yake ya Botafogo.

**#1. Cristiano Ronaldo**

Cristiano Ronaldo anaweza kuwa nafasi ya pili kwa kupiga chenga ukimwondoa Garrincha na amekuwa akiendelea kuipaisha jezi Na. 7.

Nahodha huyo wa Ureno ambaye ni mchezaji pekee wa Ulaya kufunga mabao 100 kwa timu ya taifa, mafanikio yake yalianza pale aliposajiliwa na Manchester United chini ya gwiji, Sir Alex Ferguson mwaka 2003.

Ukiacha msimu mmoja na Sporting Lisbon, Ronaldo mara zote amekuwa akivaa jezi Na. 7 kwa kipindi chake chote cha uchezaji katika klabu na timu ya taifa.

Ni mfungaji wa wakati wote wa Real Madrid na mshindi wa kihistoria kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa sasa anaendeleza kazi yake kule Juventus katika umri wake wa miaka 35.

## Nukuu

"Tumekuwa tukimwangalia Thomas [Partey] kwa muda mrefu, hivyo sasa tunafuraha kumpata mchezaji mwenye kiwango bora katika kikosi chetu. Ni kiungo wa aina yake na mwenye nguvu kubwa. Ataleta uzoefu wake hapa alioupata kwa muda mrefu kule LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya, tumeridhishwa na kiwango chake na ubora wake," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta.**



"[Edinson] Cavani hatakuwa na shida ya ukubwa wa klabu. Ni mchezaji wa kiwango cha daraja la juu, nadhani uzoefu wake utamsaidia ila macho ya watu yataelekezwa kwake na atalazimika kufanya kweli kwa sababu presha itakuwa kwake, wasiwasi wangu ni mmoja tu, wachezaji wengi wa kutoka Amerika Kusini wamekuwa na wakati mgumu wanapotua kwenye kikosi cha Man United baada ya Radamel Falcao, Angel di Maria na Alexis Sanchez kuboronga," **Gwiji wa Manchester United Ryan Giggs.**



"Kiukweli kabisa ni aibu, kwa sababu Karim [Benzema] anabaki kuwa mchezaji muhimu na mwenye ubora wake, mimi binafsi sina tatizo lolote na yeye, historia ilitaka sisi kuwa wapinzani. Mara zote nimekuwa namwelewa na namheshimu," **Olivier Giroud akisikitika Benzema kutokujumuishwa katika kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa.**



# REKODI 10 KALI LIGI KUU IKIENDA MAPUMZIKO

Na Adam Fungamwango

RAUNDI tano za Ligi Kuu Tanzania Bara zimekamilika huku timu zote wiki hii zikiwa mapumziko kutokana na kalenda za mechi za kimataifa kwa timu za taifa.

Mpaka sasa yamepatikana mabao 74 kwenye michezo 45 ambayo zimechezwa, mechi za ushindi zikiwa 37 na sare nane tu.

Rekodi zetu zinaonyesha kuwa katika mechi 45 zilizochezwa mpaka sasa, timu zimeshinda nyumbani mechi 23, na mechi 14 za ushindi zimepatikana ugenini, huku nane zikiwa sare ambazo ni mchanganyiko wa nyumbani na ugenini.

Mpaka sasa hakuna goli lolote la penalti kwenye Ligi Kuu, huku bao la kujifunga likiwa moja tu lililopatikana kwenye mechi kati ya JKT Tanzania dhidi ya Coastal Union. Kwenye mechi hiyo, Edson Katanga wa JKT Tanzania alijifunga na kuipa Coastal Union ushindi wa bao 1-0.

Zifuatazo ni rekodi nyingine kali zilizowekwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 hadi kufikia raundi ya tano, zifahamu sasa...



Washambuliaji wa Simba waliofunga mabao saba kati ya 14 ya timu hiyo, kutoka kushoto ni Chris Mugalu (mabao 3), Meddie Kagere (mabao 4). Kulia ni mpishi mkuu wa mabao wa klabu hiyo, Clatous Chama. **PICHA: MAKTABA**

**1. Azam yashinda mechi zote**

Licha ya kwamba inaongoza Ligi Kuu mpaka sasa, Azam FC ndiyo timu pekee mpaka sasa imeshinda mechi zote za ligi, ikishinda zote tano, ikiongoza kwa pointi 15, mabao tisa ya kufungwa, ikifunga mawili tu.

**2. Simba haikamatiki kwa kutupia**

Mabingwa watetezi, Simba ndiyo timu iliyofunga mabao mengi zaidi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu. Tayari imeshatupia mabao 14 kwa mechi tano tu ilizocheza, na inakamata nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 13, ikishinda mechi nne na kutoa sare moja.

**3. Yanga beki ukuta wa chuma**

Yanga inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 13 kama Simba, lakini imezidiwa mabao ya kufunga, kwani imefunga mara saba tu. Lakini mpaka sasa ina rekodi ya kuwa timu iliyofungwa mabao machache zaidi kuliko timu yoyote ile. Imefungwa goli moja tu mpaka sasa, huku Simba na Azam zenyewe zikiruhusu mabao mawili kila moja.

**4. Simba, Yanga na Azam hazijapoteza**

Timu tatu za juu, Azam inayoongoza ligi kwa pointi 15 na Simba na Yanga ambazo zina pointi 13 kila moja, ndizo timu ambazo mpaka sasa hazijapoteza mechi yoyote ile ya Ligi Kuu.

Timu hizo zimeshacheza mechi tano kila moja. Ni Azam pekee iliyoshinda zote, huku Simba na Yanga zikishinda nne na sare moja kila moja.

**5. KMC, Mwadui, Namungo hazina sare**

Jumla ya timu tano mpaka sasa hazijatoka sare yoyote ile mpaka sasa. Timu hizo ni Azam, KMC, Mwadui, Namungo na Ihefu FC.

Ni Azam tu ndiyo iliyoshinda zote, lakini zilizobaki zimeshinda na pia kupokea vichapo, kila moja ikiwa kwenye nafasi tofauti.

**6. Mbeya City haijaziona nyavu**

Timu ya Mbeya City, licha ya kwamba imeweka rekodi ya kutoshinda mechi hata moja mpaka sasa, lakini ina rekodi ya pili kuwa ndiyo timu pekee ambayo haijafunga bao hata moja kwenye Ligi Kuu mpaka sasa. Imecheza mechi tano, imetoka sare moja na kufungwa nne. Hata sare yake ilikuwa ni ya bila kufungana dhidi ya Tanzania Prisons.

7. Simba haijaruhusu bao nyumbani

Rekodi zinaonyesha kuwa Simba haijaruhusu bao lolote ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Benjamin Mkapa. Mechi ya kwanza ilicheza dhidi ya Biashara United na kushinda 4-0, ya pili dhidi ya Gwambia ikashinda 3-0, huku mechi tatu ikicheza ugenini dhidi ya Ihefu FC (Sokoine, Mbeya) ikashinda 2-1 kabla ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 (Jamhuri, Morogoro) dhidi ya Mtibwa Sugar na kisha kwenda kuichapa JKT Tanzania 4-0 katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

**8. Yanga, Azam hazijaruhusu bao ugenini**

Timu za Yanga na Azam hazijafungwa bao lolote zikicheza viwanja vya ugenini. Yanga imecheza mechi mbili ugenini na kushinda bao 1-0 kila mechi dhidi ya Kagera Sugar na Mtibwa Sugar, huku Azam ikicheza mechi mbili ikishinda bao 1-0 kila mechi dhidi ya Mbeya City na Tanzania Prisons.

**9. JKT Tanzania haijashinda nyumbani**

Timu ya JKT Tanzania haijashinda mechi yoyote ikicheza nyumbani, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, badala yake pointi zake zote nne imezipatia ugenini. Kati ya mechi tano ilizocheza, imecheza mbili nyumbani ikifungwa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji na mabao 4-0 dhidi ya Simba.

**10. Azam, Biashara vinara pointi za nyumbani**

Timu za Azam FC na Biashara United ndiyo zinaongoza kwa kuvuna pointi nyingi zikicheza viwanja vya nyumbani. Timu hizi zimevuna pointi tisa kila moja kukiwa hakuna timu yoyote yenye idadi ya pointi hizo ilizozipata ikiwa uwanja wa nyumbani.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO cha mabao 2-1 ilichokitoa kwa Ukraine juzi, kinaifanya Ujerumani sasa kupata ushindi wake wa kwanza kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya katika Kundi lao la A4. Kikosi hicho cha Joachim Low kimeshindwa kufurukuta katika mechi sita za awali ilizocheza, lakini juzi mabao ya Matthias Ginter na Leon Goretzka yaliwapa ushindi wa kwanza.





# Wafugaji waagizwa uogeshaji wa mifugo

**Na Augusta Njoji,** BAHI

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imewaagiza wafugaji kuhakikisha wanaogesha mifugo yao ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe ambayo yanachangia vifo vya ng'ombe nchini kwa asilimia 72.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizindua awamu ya tatu ya kampeni ya uogeshaji mifugo nchini iliyofanyika katika Kijiji cha Bahi Sokoni, Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma.

"Lengo la kuogesha mifugo ni kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe hususan ndigana kali ambayo imekuwa ni tatizo katika kuendeleza tasnia ya mifugo nchini, na magonjwa haya yamekuwa yakiathiri mifugo na kusababisha hasara kubwa kwa mfugaji," alisema.

Alibainisha kuwa katika vifo hivyo, asilimia 44 huchangiwa na ugonjwa wa ndigana kali.

Katibu Mkuu huyo alisema hasara inayotokana na magonjwa hayo inakadiriwa kuwa takribani Sh. bilioni 145, na kusababisha kupungua uzalishaji maziwa, nyama kutokana na kukonda, kushuka kwa thamani ya ngozi, kupoteza wanyama kazi na udumavu wa ndama.

Prof. Gabriel alisema lengo la serikali ni kuongeza tija ya ufugaji kwa kuwa na mifugo yenye afya itakayozalisha mazao zaidi yenye ubora wa kitaifa na kimataifa, ambapo uogeshaji wa mifugo kwa kutumia josho ni mzuri na unadhibiti magonjwa hayo.

Aidha, alisema mwaka 2018 wizara hiyo ilitengeneza mkakati wa kudhibiti magonjwa hayo kwa kuanzisha kampeni hiyo ambapo kwa awamu ya kwanza na pili serikali ilinunua lita 21,373.06 zenye thamani ya Sh. milioni 740.7 kwa ajili ya kuogesha mifugo.

"Katika awamu zote mbili kumekuwa na jumla ya michovyo milioni 245.37 ya mifugo yote ikiwamo ng'ombe milioni 176.32, mbuzi milioni 58.02, kondoa milioni 20.03 na punda 2,685," alisema.

Kuhusu kampeni huyo awamu ya tatu, alisema serikali imenunua dawa ya kuogesha mifugo aina ya Paranex, Paratop, Amitraz kiasi cha lita 15,579 zenye thamani ya Sh. milioni 592.82 ambazo zitatosheleza majosho 1,983 katika halmashauri 162 na michovyo inayotarajiwa ni milioni 405 ya mifugo yote itakayoogeshwa.

Aliagiza halmashauri kusimamia kanuni ya uogeshaji ili wafugaji waifuate na kushirikiana nao kujenga na kukarabati majosho na miundombinu mingine ya mifugo.

Awali, akitoa taarifa ya uogeshaji mifugo wilayani Bahi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Fatuma Mganga, alisema asilimia 55 ya mapato ya ndani ya halmashauri hiyo yanachangiwa na mifugo.

Alisema kuna minada 15 ambayo hufanyika biashara ya kuuza mifugo ambapo wastani wa ng'ombe 3,882, mbuzi 4,602 na kondoo 89 waliuzwa kwa mwezi.

Dk. Mganga alisema mzunguko wa fedha kwenye minada hiyo kwa mwezi Agosti, 2020 ni zaidi ya Sh. bilioni 2 ambazo zilitokana na mauzo ya mifugo hiyo. Hata hivyo, alisema halmashuari imekwisha andika andiko la mradi wa kiwanda cha uchakataji ngozi lenye thamani ya Sh. bilioni 3.3 tayari andiko hilo lipo Wizara ya Fedha kwa ajili ya mapitio ya mwisho kabla fedha kutolewa.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Prof. Hezron Nonga, alisema mwaka 2019, majosho zaidi ya 511 yalikarabatiwa nchi nzima kwenye halmashauri, huku 78 mapya yalijengwa. "Vifo vya ng'ombe hususan ndama vilipungua kwa asilimia 30 kwa sababu ya uogeshaji, tukiogesha vifo vya ng'ombe zetu tunatokomeza," alisema.




Baadhi ya wananchi wakitoka kununua mahitaji kwenye soko la Mavunde Chang'ombe, jijini Dodoma jana. Soko hilo, limeboreshwa na kuwa la kisasa baada ya lile la zamani lililokuwa na mapaa ya magunia kuondolewa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# EWURA: Kutakuwa na mafuta ya kutosha wakati wa uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huudma za Nishati na Maji (EWURA), imesema kutakuwa na mafuta ya kutosha nchini wakati wa shughuli za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, aliyasema hayo kwa nyakati tofauti baada ya kufanya ziara kwenye Kampuni za Uuzaji wa Mafuta Tanzania (OMCs) na kumhakikishia uwapo wa mafuta kwa kipindi hicho.

Chibulunje alisema OMCs imeihakikishia EWURA usalama thabiti wa usambazaji wa bidhaa za petroli wakati wa shughuli hizo.

"Katika ziara yangu nimekutana na watendaji wakuu wa jumla wa Total Tanzania, GBP Tanzania na Oryx Energy na wamenihakikishia kuwa watasambaza bidhaa za petroli za kutosha wakati na baada ya uchaguzi mkuu," alisema.

Aidha, alisema wakati nchi inaelekea kwenye uchaguzi huo matumizi halisi ya mafuta ya kila siku ya dizeli katika robo ya tatu ya mwaka 2020 ilifikia lita milioni 5.83 iliongezeka kutoka lita milioni 5.14 kwa mwaka 2019. Pia alisema kwa upande wa petroli imeongezeka hadi lita milioni 4.61 kutoka lita milioni 3.654 zilizopatikana mwaka 2019.

Katika ziara hiyo, Mhandisi Chibulunje alipokea maoni ya uboreshaji wa usalama na usambazaji bidhaa za mafuta, ambapo OMCs waliomba kuwadhibiti waendeshaji wengine wasio waaminifu ambao wanauza bidhaa kwa punguzo kubwa ambalo ni chini ya gharama ya bidhaa. Alisema EWURA na mamlaka zingine zinazohusika ikiwamo Tume ya Ushindani wanalichukua suala hilo ili kulitafutia ufumbuzi.

Kwa upande wao, Mkurugenzi wa Petroli, Gerald Maganga na Meneja Biashara wa Petroli, Kemi Kafanabo, walisema wako tayari kufanya kazi kwa saa nyingi zaidi ili kuhakikisha usambazaji wa bidhaa za petroli unakuwa sawa nchini.

# Viongozi wa dini waombwa kutoa elimu ya chanjo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WIZARA ya Afya Maendeleo, Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imewaomba viongozi wa dini kusaidia kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kupata chanjo kwa ajili ya kuzuia magonjwa yanayozuilika.

Mejena Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk. Dafrossa Lyimo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na viongozi wa dini wa Mkoa wa Dodoma, kwenye warsha ya kusaidia kuelimisha waumini wao umuhimu wa kupata chanjo ya kujikinga na maambukizi ya magonjwa mbalimbali yanayozuilika.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kukanusha upotoshaji unaojitokeza kuhusiana chanjo hizo zinazotolewa kuwa zina madhara kwa wanaopatiwa.

Meneja huyo alisema kuwa hofu iliyojengeka kuwa huduma hiyo kiafya siyo nzuri ni taarifa za uzushi.

Aliwaomba kutokana na ukaribu wao na waumini serikali inaamini watafikisha elimu hiyo kwa wakati na uhakika.

"Nafasi mnazokuwanazo za kila siku kukutana na waumini kupitia mikutano ya mihadhara, semina, makongamano na mtu mmoja mmoja. Ni imani yetu sisi watumishi wa Wizara ya Afya elimu hii itawafikia na wataweza kushiriki kikamilifu kwenye kupatiwa huduma ya chanjo," alisema.

Awali, akifungua warsha hiyo Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto kutoka wizara hiyo, Dk. Ahmad Makuwani, alisema mpango wa kudhibiti magonjwa yanayotibika kwa huduma ya chanjo unaridhisha kutokana na mafanikio yanayoonekana kwa kiasi kikubwa hapa nchini.

Alisema kuwa mafanikio hayo yametokana na watumishi wa afya kuwafikia jamii kwenye maeneo yao kwa wakati ikiwamo kutoa elimu na uhamasishaji wa umuhimu wa kupata chanjo.

Dk. Makuwani alitaja baadhi ya magonjwa ambayo yaliyodhibitiwa kwa kiasi kikubwa kwa kutibiwa na chanjo ni pamoja na surua, polio, tetenas na kifaduru ambayo kwa hivi sasa hapa nchini Tanzania imefanikiwa kupungua kwa kiasi kikubwa.

"Kwa kushirikiana na nyinyi maaskofu, mashehe na wachungaji ni tumaini letu sisi kama wizara ya afya tunaamini elimu mtakayopewa hapa mtakuwa mabalozi kwa waumini wenu, ili na wao waone umuhimu wa kupata chanjo ili kujikinga na maambukizi ya magonjwa mbalimbali," alisema.





## Mgombea aahidi kusimamia ruzuku kwa wakulima

**Grace Mwakalinga,** MBARALI

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mbarali, mkoani Mbeya, kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Francis Mtega, ameahidi kusimamia utoaji wa ruzuku kwa wakulima kwa kuzingatia masharti nafuu pamoja na uhakika wa soko la zao la mpunga.

Mtega alitoa ahadi hiyo jana kwenye mkutano wake wa kampeni uliofanyika kwenye Kata ya Igurusi, kuwa jukumu la kwanza atakalolifanya kama atachaguliwa kwenye uchaguzi mkuu ni kusimamia utoaji wa ruzuku za pembejeo za kilimo kwa masharti nafuu ili kumsaidia mkulima kuzipata kwa wakati.

Alisema Kata ya Igurusi ni moja ya maeneo ambayo wakazi wake kwa asilimia kubwa wanajihusisha na kilimo hivyo wanapaswa kuandaliwa mazingira bora ya kufanya shughuli zao.

"Mkinichagua kuwa mbunge wenu nitashughulikia suala la utoaji ruzuku za pembejeo za kilimo kama vile mbolea, kwa kuhakikisha zinauzwa kwa bei elekezi na mtakayoweza kuimudu, lakini pia ipatikane kwa wakati na mara nyingine kuuzwa kwa bei ghali, mimi ni mkulima na madhira hayo yananigusa moja kwa moja mnichague ili nikayasemee hayo kwa watunga sheria na sera," alisema Mtega.

Alisema atahakikisha kunapatikana wataalamu wa kutosha kwenye kilimo na ufugaji ili wawasaidie wakulima kuwapa mbinu za kuzalisha kwa tija na kuendana na soko la kimataifa na kuwafundisha wafugaji namna bora ya kufuga mifugo michache yenye manufaa, ili kuepuka uharibifu wa mazingira na migogoro ya ardhi. Mgombea udiwani wa Igurusi, Hawa Kihwele alisema moja ya matatizo yanakabili eneo hilo ni barabara na madaraja hali inayosababisha maafa na vifo.

Alisema kipindi cha masika baadhi ya madaraja hayapitiki na kusababisha wanafunzi kushindwa kuhudhuria vipindi vya masomo.Alimwomba mgombea ubunge, Francis Mtega, akipewa ridhaa ya kuongoza na Wanambarali kushughulikia matatizo ya miundombinu ili wakazi wa eneo hilo waishi kwa furaha.

Akijibu hoja hizo, Mtega aliwahakikishia Wanaigurusi kuwa atazungumza na Wakala wa Huduma za Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Mbarali kuhusu ukarabati wa barabara na madaraja katika vijiji vya Muungano, ili kuunganisha mawasiliano na kuweka alama za pundamilia kwenye barabara kuu ya Mbeya-Iringa ili kuzuia ajali za mara kwa mara.

Naye mwanachama wa chama hicho Mkoa wa Mbeya, Sauli Mwaisenye, aliwaomba wananchi kuchagua viongozi walio tayari kutatua matatizo yanayowakabili.

# Aina mpya mbegu ya ulezi kupunguza udumavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania TARI, Kituo cha Uyole kilichopo mkoani Mbeya, kimebuni aina tatu za mbegu za ulezi zenye madini ya protini, kalsiamu na virutubisho vingine muhimu kwa ajili ya afya ya mwanadamu ili kukabiliana na tatizo la udumavu na kisukari kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu Wiki ya Chakula Duniani iliyoanza Oktoba 10 ikibeba kaulimbiu: 'Kesho njema hujengwa na lishe endelevu', Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema aina mpya za mbegu za ulezi zitasaidia kupunguza tatizo la udumavu pamoja na utapiamlo katika jamii.

Dk. Bucheyeki alisema mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inakabaliwa na tatizo kubwa la utapiamlo pamoja na udumavu licha ya kuwa inaongoza kwa uzalishaji mkubwa wa chakula.

Alisema mwarobaini wa tatizo la udumavu na utapiamlo ni ulezi na kwamba wananchi wanapaswa kutumia uji wa zao hilo kwa kuwa una virutubisho vyote muhimu katika kukabiliana na magonjwa.

"Kituo chetu kimebuni teknolojia mpya za mbegu za ulezi ambazo zililenga kuboresha afya za wananchi wetu, tunataka kukomesha tatizo la udumavu na utapiamlo dhidi ya watoto, lakini hata watu wazima maana ulezi unavirutubisho vinavyohitajika kwa ajili kuimarisha afya za wananchi," alisema Dk. Bucheyeki.

Mtafiti wa zao la ulezi Kituo cha Uyole, Dk. Dennis Tippe, alisema jukumu la kituo hicho ni kuhakikisha lishe za wananchi zinaendelea kuimarika kupitia aina mpya za mbegu walizozibuni ili kukabiliana na tatizo la udumavu.

Alisema kwenye Wiki ya Chakula Duniani ambayo ilianza Oktoba 10 hadi 16, kituo hicho kitajikita kutoa elimu na umuhimu wa ulezi kwa kuhamasisha matumizi ya uji.

Alisema tayari kituo hicho kimeanza kupika uji kwa kuhakikisha watumishi wote wanajenga utamaduni wa kunywa kinjwaji hicho.



Daktari wa macho kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Fariji Killewa, akimfanyia uchunguzi wa macho mmoja wa wagonjwa, wakati wa kilele cha Siku ya Afya ya Macho Duniani, iliyofanyika hospitalini hapo, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mahakama Kuu yaboresha huduma kutoa haki

**Na Grace Mwakalinga**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania imeanzisha utaratibu wa kuboresha huduma zake ikiwamo kusikiliza na kuamua mashauri kwa wakati na kutoa nakala za hukumu lengo likiwa ni kutoa haki kwa wakati.

Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa jengo jipya la Mahakama ya Wilaya ya Chunya.

Alisema mwaka huu, mahakama imejipambanua kusimamia maadili ya watumishi wa umma kwa kuhakikisha wanasimamia na kuendesha mashauri kwa muda uliopangwa na kutumia teknolojia ili kurahisisha kazi.

"Kuna tatizo la kuchelewa kusikiliza kesi na utoaji wa maamuzi kwa wakati katika kuboresha mahakama tayari iliandaa utaratibu wa kushughulikia kisasa, ambapo tunatumia teknolojia ili kuwapatia wananchi huduma bora," alisema Dk. Feleshi.

Alisema licha ya serikali kuendelea kusogeza huduma, utoaji wa sheria katika kila pembe ya nchi kwa kufungua na kuboresha miundombinu ya mahakama, aliwataka watumishi kuwa waadilifu na wazalendo. "Nawasihi watumishi wa mahakama hii ya Chunya na nyingine za hapa nchini kubadili mienendo na tabia ambazo zimekuwa zikikiuka miiko na maadili ya kazi kwa watumishi wa umma kama vile rushwa na matumizi mabaya ya lugha," alisema Jaji Kiongozi.

Akisoma risala kwa mgeni rasmi, Mtendaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Teoford Ndomba, alisema kukamilika kwa jengo hilo ni hatua kubwa za kufanikisha maboresho ya miundombinu ya mahakama, pia kutasaidia kuimarisha huduma ya kimahakama katika Wilaya ya Chunya na kujenga imani kwa watoa huduma za kimahakama. Alisema jengo hilo limegharimu Sh. milioni 443.

# Shein ataka usimamia malezi ya watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wazee kuendelea kusimamia malezi ya watoto wao, wakati huu vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vikiwa vimeshamiri.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa Shule ya Sekondari Mwanakwereke mpya, ambayo hivi sasa inatambulika kwa jina la Shule ya Sekondari ya Dk. John Pombe Magufuli.

Alisema vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambavyo vimeshamiri sio sifa ya Wazanzibari, hivyo akawataka wazee kutoiachia serikali pekee jukumu la kukabiliana na uhalifu huo na badala yake kushirikiana nayo.

"Hali hii ni lazima tushikamane katika kupambana na wahalifu hao," alisema Dk. Shein.

Alieleza kuwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto wadogo, ikiwamo wanafunzi vimekuwa vikifanywa kwa makusudi, huku familia zinazoathirika zikiwaficha wahalifu wanaohusika.

Dk. Shein alisema anaunga mkono azma ya mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi, ya kuchukua hatua kali katika kukabiliana na vitendo hivyo.

Alisema serikali inaendelea na juhudi za kuweka mazingira bora ya elimu ili kupata wataalamu wazalendo na ndio maana shule zinazojengwa kama hiyo zimekuwa na maabara za aina tofauti.

Aidha, aliwataka wanafunzi kusoma kwa bidii, huku serikali ikiendelea na jukumu lake la kuweka mazingira bora, ikiwamo kufanikisha dhana ya elimu bila malipo na kutoa elimu bure hadi kidato cha sita kadri uchumi utakavyoendelea kukua.

"Nyinyi wanafunzi kazi yenu kusoma, serikali yenu iko pamoja nanyi na walimu nanyi somesheni kwa kutengeneza sio kulipua, na wazee simamieni maendeleo ya elimu ya watoto wenu," alisema.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema wizara hiyo itaendelea kusimamia maendeleo ya elimu nchini na kuhakikisha ubora wa elimu unasimamia vizuri.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idrissa Muslim Hijja, alisema hadi kufikia mwaka 2010, Zanzibar ilikuwa na jumla ya shule 10 za sekondari za majengo ya ghorofa, ikiwamo Lumumba, Haile Sellasie, Ben-bella, Hamamni, Forodhani, Tumekuja, Uwelení, Kiponda, Hurumzi na Mwanakwerekwe 'C'.

Alisema katika kipindi cha miaka kumi ya uongozi wa awamu ya saba chini ya Dk. Shein, jumla ya shule 26 za sekondari za majengo ya ghorofa zimejengwa.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Anna Msuya, akimnadi mgombea ubunge wa Jimbo la Kikwajuni, Hamad Yussuf Masauni, katika mkutano wa kampeni kwenye viwanja vya Kisonge, mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Kada awapigia debe wagombea wa CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Anna Msuya, amewataka wananchi wa Zanzibar kuwachagua wagombea kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi mkuu unatarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Alisema hayo alipokuwa akihutubia mkutano wa kampeni Jimbo la Kikwajuni uliofanyika katika uwanja wa kisonge Mjini Unguja, na kuwanadi kuwaombea kura wagombea wa jimbo hilo kupitia CCM.

Msuya alisema ni vyema wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kuhakikisha wanawarudisha tena madarakani viongozi wa jimbo hilo kutokana na maendeleo makubwa waliyoyafanya katika kipindi cha uongozi wao sambamba na kuwahimiza katika kufanikisha ushindi wa CCM kwa kiti cha urais na majimbo yote.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na serikali inayoongozwa na CCM ni moja ya alama ya kuwa chama hicho kinatoa viongozi bora na wenye uzalendo wa kuleta maendeleo.

Akiomba kura kwa wananchi wa Kikwajuni mgombea ubunge wa jimbo hilo, Mhandisi Hamad Masauni, aliwahakikishia wananchi kuwa amechochea maendeleo makubwa katika awamu iliyopita, ikwamo kutatua changamoto ya upatikanji wa majisafi na salama.

Masauni pia aliwaahidi wananchi wa jimbo hilo, kuwa kipindi kijacho endapo atapata ridhaa tena ya kuongoza, atahakikisha anakabiliana na changamoto ya ajira kwa wananchi wa Kikwajuni.

"Katika kipindi cha uongozi wangu niliahidi kukabiliana na tatizo la maji na tayari nimefanikiwa kwa kuchukua juhudi mbalimbali ikiwamo kuanzisha miradi ya upatikanaji wa maji jimboni yenye gharama ya zaidi ya bilioni moja kwa ushirikiano na wafadhili mbalimbali ndani na nje ya nchi, na kwasasa endapo mtatupa ridhaa ya kuongoza tena, nitahakikisha tunakabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira ili kupunguza idadi ya wimbi kubwa la vijana ambao hawana ajira," alisema Masauni.

Wagombea wengine wa Jimbo la kikwajuni ni Nassor Salum Jazeera anayegombea nafasi ya uwakilishi, Ibrahim Khamis, nafasi ya udiwani Wadi ya Kikwajuni na Mbarouk Abdulla Hanga, nafasi ya udiwani Wadi ya Rahaleo.

# Mwelekeo wa TASAF wairidhisha SMZ

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umeonyesha mwelekeo mzuri wa ufanisi mkubwa unaopatikana katika utekelezaji wa miradi ya jamii tokea ulipoanzishwa ndani ya awamu ya tatu ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Alisema viongozi wa wilaya, halmashauri, majimbo, wadi na shehia wana wajibu na jukumu la kuwasimamia vyema wananchi katika kuona miradi wanayoiibua katika maeneo yao inaendelea kupata ufanisi kama inavyojidhihirisha hivi sasa katika mpango huo unaosaidia kustawisha jamii.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na walimu, wanafunzi na wananchi wa shehia za Mkataleni na Mahonda, baada ya kuweka mawe ya msingi ya ujenzi wa jengo la madarasa matatu pamoja na jengo la utawala la Shule ya Sekondari ya Mahonda, miradi inayofadhiliwa na TASAF.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililazimika kufanya mabadiliko katika ngazi ya utawala kwenye mfuko wa TASAF kwa upande wa Zanzibar, ili taasisi hiyo ya kijamii inatekeleza wajibu wake katika misingi iliyopangiwa ya kuunga mkono jitihada za jamii kwenye miradi yao ya maendeleo.

Balozi Iddi alisema wapo baadhi ya watendaji wa TASAF katika kipindi kilichopita walikuwa wakizorotesha kazi kwa kufikiria zaidi maslahi yao binafsi bila kujali kwamba chombo hicho kimeanzishwa kwa lengo la kuwakomboa wananchi kiuchumi.

"Nikiri kwa dhati kwamba majengo haya niliyoyawekea mawe ya msingi hivi punde yanaendelea kujengwa katika ubora unaokubalika katika fani ya ujenzi, na uharaka wake uliyofikia huwezi kuamini kama ni ya mwezi mmoja," alisema Balozi Iddi.

Alisema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia sera yake ya elimu imejizatiti kuona wanafunzi wote wa visiwa vya Unguja na Pemba wanapata taaluma katika mazingira bora na kiwango kinachokubalika kitaifa na kimataifa. Akisoma risala ya wananchi wa shehia za Mahonda na Mkataleni, mjumbe wa kamati ya usimamizi wa ujenzi wa majengo hayo, Madaraka Suleiman Haroun, alisema ushiriki wa wananchi katika ujenzi huo umeleta faraja kubwa licha ya kuwapo baadhi yao kuona mradi huo hauwahusu.

Madaraka alisema kukamilika kwa miradi hiyo miwili kutasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi na hata walimu, jambo ambalo litaongeza fursa za masomo zitakazokwenda sambamba na ufaulu mkubwa utakaosaidia kurejesha heshima ya shule hiyo.

Wakitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga na Mkurugenzi wa Uratibu wa Shughuli za Serikali Zanzibar anayesimamia TASAF, Khalid Bakari Amran, walisema Zanzibar imepangiwa kupata Sh. bilioni 112 katika kipindi cha miaka minne ijayo.

Walieleza kwamba utekelezaji wa mradi wowote wa TASAF hupangiwa kukamilika ndani ya kipindi kisichozidi miezi 12, lakini itashangaza kuona miradi inayotekelezwa ndani ya Zanzibar haizidi katika kipindi cha miezi minne, ukiwa ni mfano bora.

## HABARI PICHANI

# HEKA HEKA KAMPENI ZA UCHAGUZI MKUU



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati akimwombea kura mgombea urais wa CCM, Rais Dk. John Magufuli, mbunge na madiwani wa CCM katika mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye uwanja wa Burwa, Amani wilayani Muheza Mkoa wa Tanga, jana. **PICHA: OWM**



Mgombea urais kuptia Chama cha ADC, Queen Cuthbert Sendiga, akihutubia wananchi wa Tandahimba Mjini mkoani Mtwara jana, ikiwa ni hitimisho la kampeni zake kwa upande wa mikoa ya kusini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shy-Rose Bhanji (kushoto), akimnadi mgombea urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli katika maeneo mbalimbali ya Mbweni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mgombea ubunge Jimbo la Ukonga kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Webiro Wassira (katikati), akizungumza na baadhi ya wakazi wa Kitunda Kati wakati alipokuwa katika mkutano wa kampeni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA:JUMANNE JUMA**



Mgombea ubunge wa Jimbo la Vunjo mkoani Kilimanjaro (CCM), Dk. Charles Kimei, akipokea baraka za wakazi wa Kata ya Marangu Magharibi juzi, baada ya Agness Makombe kumwekea mikono kichwani ili kumtakia ushindi, wakati wa mkutano wake wa kampeni za kujinadi kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu. **PICHA: GODFREY MUSHI**



Mbunge mteule wa Jimbo la Babati Vijijini mkoani Manyara, kwa tiketi ya CCM, Daniel Sillo, akiomba kura za mgombea urais na madiwani kwenye Kijiji cha Saydoda Kata ya Ufana, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

HABARI KIMATAIFA

# Maambukizi corona yapaa zaidi Ulaya, Amerika Kusini

**Bonn, Ujerumani**

UJERUMANI na Poland zimeweka upya masharti ya karantini ili kudhibiti kuenea maambukizi ya virusi vya corona.

Idadi ya watu wanaoambukizwa imeendelea kuongezeka baranı Ulaya,

Karantini imewekwa kwenye mji mkuu wa Ujerumani, Berlin maarufu kwa shughuli za usiku ili kukabiliana na kusambaa kwa virusi vya corona.

Migahawa na baa vitafungwa saa tano usiku, marufuku ambayo itadumu hadi Oktoba 31.

Hatua kama hiyo imechukuliwa katika mji wa Frankfurt, lakini utekelezaji wake utaanza saa nne usiku huku kukiwa na maambukizi ya zaidi ya watu 400 kwa siku mjini Berlin.

Pia ufungaji wa maeneo hayo ya biashara unahusu maduka yote isipokuwa maduka ya dawa na vituo vya kuuzia mafuta ingawa havitaruhusiwa kuuza pombe.

Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel tayari alionya siku ya Ijumaa wiki iliyopita, kuwa maeneo yenye kiwango kikubwa cha maambukizi yataangaliwa kwa muda wa siku 10 kuona kama maambukizi yatapungua la sivyo hatua madhubuti zitachukuliwa.

Katika nchi jirani ya Poland, viongozi wanawasisitizia watu wavae barakoa katika maeneo yote ya umma baada ya maambukizi mapya ya virusi hivyo kwa siku moja kufikia watu 4,280.

Jamuhuri ya Czech, matarajio ya kuwekwa vizuizi vipya yanapewa kipaumbele kutokana na kuongezeka kwa maradhi ya COVID -19.

Serikali mbalimbali barani Ulaya, zinajitahidi kudhibiti kuongezeka kwa maambukizi wakati huu wa wimbi la pili la janga la corona linalotokea huku msimu wa mafua makali (Influenza) ukiwa unasubiriwa.

Shirika la Afya Duniani (WHO), limesema kwa mara ya kwanza idadi ya kila siku barani Ulaya ya maambukizi ya virusi vya corona imefikia watu 100,000 huku Hispania ikiathirika zaidi kutokana na maambukizi hayo.

Serikali ya nchi hiyo imetangaza hali ya dharura katika mji mkuu, Madrid.

Miji kadhaa ya Ufaransa tayari imeshashuhudia idadi ya kupindukia ya maambukizi hayo na Uholanzi, zaidi ya maambukizi mapya ya watu 6,000 yaliripotiwa, huku idadi ya wagonjwa ikiwa inaongozeka mahospitalini.

Wakati huo huo, Daktari wa ikulu ya Marekani, Kamanda Sean Conley, alisema, Rais Donald Trump, hayumo tena katika kitisho cha kuweza kuambukiza virusi vya corona.

Taarifa hiyo ya uchunguzi wa kitabibu ilitolewa katika kipindi ambacho Rais Trump anajiandaa kuanzisha upya kampeni na shughuli zingine.

Taarifa ya daktari huyo ilisema Trump ametimiza vigezo vya usalama kulingana na Kituo cha Udhibiti na Kinga (CDC) kwa hiyo hayumo katika hatari ya kuweza kueneza maambukizi.

Taarifa hiyo ilitolewa baada ya Rais Trump kuonekana kwa mara ya kwanza mbele ya umma, tangu aliporudi Ikulu baada ya kutibiwa ugonjwa wa COVID -19.

Mamia ya watu walikusanyika siku ya Jumamosi alasiri kwenye eneo la wazi la Kusini mwa Ikulu wakati Rais Trump akiwa kwenye roshani aliwahutubia na kusisitiza kuhusu anavyowaunga mkono maofisa wa usalama nchini Marekani. DW



Madaktari wakiwa kwenye chumba cha wagonjwa mahututi wanaougua COVID -19 nchini Ufaransa. Idadi ya watu wanaoambukizwa virusi vya corona imeendelea kuongezeka barani Ulaya. **PICHA: DW**

# Tishio la ubakaji wanawake India

**Dalit, India**

WIKI iliyopita, inasemekana kwamba mwanamke wa Dalit (19), alibakwa na genge la wahalifu na kushambuliwa na kundi la wanaume wa tabaka la juu kutoka Jimbo la Uttar Pradesh.

Taarifa hizo zinaonyesha kusambaa kwa dhuluma za kingono kunakowakabili wanawake milioni 80 wa Dalit nchini India na waume zao ambao nao pia wanachukuliwa kuwa wa tabaka la chini kabisa.

Wanawake hao ambao ni karibu asilimia 16 ya idadi ya wanawake nchini India, wanakabiliana na 'mzigo mara tatu' wa ubaguzi wa kijinsia, kunyanyapaliwa na ukosefu wa mahitaji ya msingi.

"Wanawake wa Dalit wanatoka katika kundi linalonyanyaswa zaidi duniani," alisema daktari Suraj Yengde, mwandishi wa kitabu cha 'Caste Matters'.

"Ni mwathirika wa utamaduni na unyanyasaji wa taasisi, ndani na nje. Na hili linajitokeza katika dhuluma ambazo wanawake wa Dalit wamekuwa wakizipitia miaka nenda rudi."

Matokeo ya ubakaji uliotokea hivi karibuni na mauaji ya mwanawake wa Hathras, huko Uttar Pradesh, yanayosemekana kutekelezwa na wanaume wa tabaka la juu, kulionyesha hali inayoshuhudiwa pale mwanamke wa Dalit anaposhambuliwa:

Polisi wamerekodi malalamishi kwa kasi ya polepole; wachunguzi huchukua muda mrefu; maofisa huanza kushuku, ikiwa kweli ubakaji umetokea; kuna dhana kwamba hilo halina uhusiano wowote na tabaka; na mamlaka huonekana kuunga mkono tabaka la juu ambao ndio watendaji wa dhuluma hizo.

Wanawake 10 wa Delit walibakwa kila siku nchini India, mwaka jana, kulingana na idadi rasmi iliyotolewa.

Jimbo la Kaskazini mwa Uttar Pradesh, linaloongoza kwa idadi ya juu ya matukio dhidi ya wanawake pamoja na visa vya unyanyasaji vya kingono kwa wasichana.

Majimbo matatu - Uttar Pradesh, Bihar na Rajasthan - yaliripoti zaidi ya nusu ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake wa Dalit.

Kituo cha kundi la kutetea haki za wanawake wa Dalit kilitathmini matukio 100 ya dhuluma za kingono dhidi ya wanawake na wasichana wa Dalit katika maeneo 16 nchini India kati ya mwaka 2004 na 2013.

Kituo hicho kilibaini kwamba asilimia 46 ya waathirika walikuwa na umri wa chini ya miaka 18 na asilimia 85 walikuwa chini ya miaka 30. Waliotekeleza dhuluma hizo walitoka katika matabaka 36 tofauti tofauti ikiwamo tabaka la Dalit.BBC

## Saba wafa Azerbaijan kwenye mashambulizi

**Ganja, Azerbaijan**

AZERBAIJAN imesema kuwa mashambulizi yaliofanywa na vikosi vya Armenia katika mji wa pili mkubwa nchini humo Ganja, yamesababisha vifo vya watu saba siku moja baada ya makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya pande hizo mbili kutarajiwa kutekelezwa.

Katika ujumbe kupitia ukurasa wa twitter, Wizara ya Mambo ya Nje ya Azerbaijan ilisema kuwa shambulizi jipya la makombora lililofanywa na vikosi hivyo vya Armenia katika mji huo wa Ganja pia lilisababisha kujeruhiwa kwa watu wengine 33 ikiwa ni pamoja na watoto.

Hata hivyo, Wizara ya Ulinzi ya Armenia ilisema kuwa vikosi vya nchi hiyo katika eneo lililojitenga la Nagorno Karabakh vinaheshimu makubaliano hayo ya kusitisha mapigano na kuishutumu Azerbaijan kwa kuyalenga maeneo ya raia na kwamba ripoti za kushambuliwa kwa Ganja ni za uongo.

Makubaliano hayo ya kusitisha mapigano ambayo yameendelea kwa wiki mbili sasa, yalianza kutekelezwa jana Jumamosi mchana na kuidhinishwa na mawaziri wa mambo ya nje wa pande hizo mbili katika mfululizo wa mazungumzo yaliosimamiwa na Urusi mjini Moscow.

**DW**

## Waandamana kupinga ukatili wa polisi Nigeria

**LAGOS, Nigeria**

MAANDAMANO ya nchi nzima dhidi ya ukatili wa polisi yamelikumba taifa la Nigeria kwa siku ya tatu mfululizo.

Mtu mmoja anaaminika kufariki hapo juzi huku ghasia zikiendelea kati ya waandamanaji na maofisa wa polisi.

Maandamano hayo yalitarajiwa kuwa ya amani, waandamanaji walishambulia kituo cha polisi na kusababisha kifo cha ofisa mmoja wa polisi.

Polisi walifyatua gesi za kutoa machozi na pia kuwarushia magurunedi waandamanaji hao ambao waliwashtumu maofisa hao kwa kutumia risasi za moto.

Mamia ya watu waliandamana na kutoa wito wa kuvunjiliwa mbali kwa kikosi maalumu cha kukabiliana na waporaji kinachojulikana kama SARS.

Maandamano hayo yalisababisha kusitishwa kwa shughuli katika mji mkubwa wa Nigeria Lagos pamoja na mji mkuu Abuja, na miji mingine midogo. **DW**



# BRUYNE

## AIPA NAFASI ENGLAND KUBEBA EURO, KOMBE LA DUNIA

**LONDON, England**

NYOTA wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne anaamini England inatakiwa kuongoza kuwa timu inayopewa nafasi kubwa ya kutwaa Kombe la Mataifa ya Ulaya, Euro, na Kombe la Dunia mwaka 2022.

Kiungo huyo wa Manchester City jana Jumapili alikuwa sehemu ya kikosi cha Ubelgiji kilichoivaa England kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA katika Uwanja wa Wembley.

Timu zote mbili zilifika nusu fainali ya Kombe la Dunia nchini Urusi miaka miwili iliyopita.

"Nafikiri watakuwa na hamasa kubwa," alisema akiizungumzia England. "Ni timu yenye vijana wengi na wana nafasi kwa hilo."

England bado haijawahi kushinda mashindano makubwa tangu walipotwaa Kombe la Dunia mwaka 1966, lakini De Bruyne, ambaye msimu uliopita alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu ya England amesema: "Nafikiri wanatakiwa kujiwekea malengo ya kushinda mashindano ya Euro na Kombe la Dunia.

"Nafikiri wana nafasi hiyo. Mara zote kuna timu nyingi ambazo hutaka kushinda, lakini kwa timu waliyonayo, wachezaji wanaocheza katika klabu kubwa, wanatakiwa kufanya hivyo."

## LOW HAJARIDHIKA NA KIWANGO UJERUMANI

**KIEV, Ukraine**

KOCHA Mkuu wa Ujerumani, Joachim Low, bado hajaridhishwa na kiwango cha timu yake licha ya ushindi wa 2-1 walioupata dhidi ya Ukraine kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Ujerumani ilisherehekea ushindi huo kwa mabao ya Matthias Ginter na Leon Goretzka mchezo uliopigwa mjini Kiev, Jumamosi.

Ujerumani iliongoza kwa 2-0 baada ya dakika 49 kabla ya Ruslan Malinovskiy kuifungia Ukraine dakika ya 76 kwa mkwaju wa penalti.

Baada ya kushinda mchezo wake huo wa kwanza kwa mwaka huu 2020, akiwa ametoka sare mechi tatu zilizopita, Low aliwaambia waandishi wa habari: "Nina furaha kwamba tumeshinda.

"Kabla tuliruhusu mabao, tungeweza kushinda 3-0 au 4-0. Penalti haikuwa na umuhimu wowote. Jambo la muhimu ni kwamba tuliwaruhusu wapate nafasi chache za kucheza.

"Tulijitahidi, lakini haikuwa kazi rahisi sana. Walijaribu wakati tulipokuwa tunaongoza kwa mabao 2-0.

"Hata hivyo, bado tunatakiwa kufanya vizuri zaidi, maana naona uwezo huo tunao na tunaweza kwenda mbele zaidi.

"Sitabadilisha kikosi cha kwanza dhidi ya Uswisi kama hakutakuwa na majeruhi yeyote."





## ENRIQUE: HISPANIA IMESTAHILI USHINDI

**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Hispania, Luis Enrique amesema kikosi chake kilicheza kwa kujituma dhidi ya Uswisi ndio maana wakapata ushindi na sio makosa ya wageni wao hao.

Hispania iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Uswisi mjini Madrid, Jumamosi mfungaji akiwa Mikel Oyarzabal katika dakika ya 14.

Straika huyo wa Real Sociedad aliuwahi mpira wa pasi fupi uliopigwa na Yann Sommer na kuwazawadia Hispania nafasi hiyo ya kufunga kwa urahisi.

Wakati Uswisi wanaweza kulaumu makosa ya Sommer kwa bao hilo, Enrique anaamini Hispania ilipata ushindi iliostahili.

"Hayakuwa makosa yao, ilikuwa ni juhudi zetu za kucheza kwa kujituma kuanzia dakika ya kwanza ya mchezo," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafasi iliyopatikana ni kutokana na timu kucheza kwa ari kubwa na kufuta kila nafasi ya kufunga na ilipopatikana tukaitumia na si makosa ya Uswisi.

"Nafikiri hakuna ambacho sikukipenda kuhusu kiwango cha wachezaji. Maana Uswisi ni timu yenye presha kubwa, ambao wana washambuliaji wakati watatu na viungo wawili."

Hispania itacheza na Ukraine kesho Jumanne kwenye mchezo mwingine wa Ligi ya Mataifa ya UEFA.




# LUKAKU

## AITABIRIA MATAJI MENGI INTER

**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku anaamini Inter Milan ina nafasi ya kumaliza ukame wa mataji msimu huu kwa sababu ya mipango ya kocha, Antonio Conte.

Straika huyo wa zamani wa Manchester United, Lukaku amesema kufanya kazi na Conte kumeimarisha kiwango chake, akibainisha kwamba anajiona kama ni mtu aliyebadilika tangu alipohamia hapo San Siro.

Mbio zao za ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu uliopita zilitibuliwa na Juventus ambao walitwaa taji hilo kwa kuwazidi pointi moja tu.

Inter pia ilitinga fainali ya Kombe la Ligi ya Europa ambapo walifungwa na Sevilla 3-2, na hawajashinda taji lolote kubwa tangu msimu wa 2010-11 walipotwaa Coppa Italia.

Shaka juu ya majaliwa ya Conte yalifuata baada ya kumaliza msimu bila taji kabla ya baadaye kuhakikishiwa kuendelea kuwa kocha wa kikosi hicho na Lukaku anavutiwa zaidi na mbinu za kocha huyo wa zamani wa Juventus, Italia na Chelsea.

"Tangu niwe na Conte kiwango changu kimeimarika zaidi katika kila mchezo," alisema Lukaku, ambaye alitajwa kuwa mchezaji bora wa mashindano ya Ligi ya Europa msimu wa 2019-20.

"Kama unataka kucheza chini yake, lazima ujue namna ya kujitolea kwa ajili ya timu na uwe fiti.

"Mbinu zake zimenifanya niimarike zaidi kama mchezaji na nina uhakika sasa ana nafasi kubwa ya kumaliza ukame wa mataji hapa Inter Milan."

## FATI MCHEZAJI BORA WA LALIGA SEPTEMBA

**BARCELONA, Hispania**

ANSU Fati ameshinda tuzo ya Septemba kama mchezaji mwenye thamani kubwa kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Fati mwenye umri wa miaka 17, alitwaa tuzo hiyo Jumamosi baada ya kuwa na mwanzo mzuri wa msimu huu.

Katika Twitter ya mdhamini wa LaLiga, Santander, iliandikwa: "Tuna mshindi mpya mwenye thamani zaidi wa LaLiga Septemba (MVP).

"Amechaguliwa mmoja ni Ansu Fati. Hongera!"

Fati alicheza mchezo mmoja tu wa LaLiga Septemba, baada ya Barcelona kuchelewa kuanza msimu wa ligi kutokana na kuwapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Hata hivyo, mshambuliaji huyo kinda alikuwa na mchango mkubwa wakati alipofunga mara mbili ndani ya dakika 20 za mwanzo kwenye ushindi wa 4-0 dhidi ya Villarreal pale Camp Nou.

Akafunga tena siku nne baadaye, Oktoba Mosi kwenye ushindi wa 3-0 dhidi ya Celta Vigo.

Fati pia akawa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuifungia Hispania wakati akiwa na umri wa miaka 17 na siku 311, alipopachika bao kwenye ushindi wa 4-0 dhidi ya Ukraine, Septemba 6 katika mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Wakati nyota wa Barcelona, Lionel Messi akiwa amefunga bao moja tu katika mechi tatu za LaLiga msimu huu, Fati ndiye anayeongoza kwa ufungaji katika kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Mholanzi Ronald Koeman.

## Pepe kucheza Kombe la Dunia 2022 na miaka 39

**LISBON, Ureno**

MLINZI wa Ureno, Pepe anatazamia kucheza michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka 2022, wakati atakapokuwa na umri wa miaka 39.

Mlinzi huyo wa zamani wa Real Madrid, kwa sasa anacheza pale FC Porto, na amecheza mechi 111 kwa Ureno tangu alipoanza kuichezea kwa mara ya kwanza mwaka 2007.

Amecheza katika michuano mitatu ya Kombe la Dunia na mitatu ya Mataifa ya Ulaya, Euro, ikiwamo wakati wanashinda Kombe la Euro 2016 nchini Ufaransa.



Pepe alitajwa nyota wa mchezaji kwenye fainali wakati walipocheza na wenyeji na kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

Ushindani wa namba kwenye kikosi cha Ureno umekuwa mkubwa kwake, na alianza kwenye sare ya bila kufungana na Hispania, Jumanne.

Na sasa Pepe amejiandaa kucheza Kombe la Dunia, ambapo itaanza miezi mitatu kabla hajatimiza umri wa miaka 40 mwaka 2022.

"Huwezi kujua," aliwaambia waandishi wa habari kuelekea mchezo dhidi ya Ufaransa kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA.

"Kwa sasa akili yangu ni kuangalia mchezo unaofuata, lakini nafasi ya kucheza Kombe la Dunia ni kubwa kwangu."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POCHETTICHO SASA LULU KWA MAN UNITED, CITY

Solskjaer anaweza kutimuliwa kama atafungwa mechi ijayo, na Guardiola hajasaini mkataba mpya, hivyo...

**MANCHESTER, England**

MAURICIO Pochettino anaweza kujikuta akirudi tena kwenye kazi ya ukocha hivi karibuni zaidi tofauti na ilivyofikiriwa.

Pochettino alifukuzwa katika Klabu ya Tottenham Hotspur Novemba mwaka jana, akiwa ametoka kuiongoza kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19.

Sasa Manchester United na Manchester City zimeripotiwa kwamba zinawania saini ya Pochettino ili kukabidhiwa mikoba ya timu zao.

Klabu hizo za jiji moja la Manchester, zinaonekana Pochettino ndiye chaguo lao la kwanza kama wataachana na makocha wao wa sasa, kwa mujibu wa gazeti la Mirror.

Pochettino hajawa na kazi tangu alipofukuzwa kule Tottenham na anapewa nafasi kubwa ya kwenda kuchukua mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer ambaye yupo kwenye nafasi ngumu pale United.

Kikosi hicho cha Solskjaer kilifumuliwa mabao 6-1 na Spurs kwenye mchezo wa Ligi Kuu kabla ya mechi za kimataifa.

Makamu Mwenyekiti wa United, Ed Woodward, ameripotiwa kwamba yupo tayari kumfukuza Solskjaer kama matokeo hayataimarika ndani ya kikosi hicho.

Imeripotiwa kwamba, Solskjaer anaweza kupoteza kibarua chake kama atafungwa kwenye mechi ijayo ya Ligi Kuu.

Wakati huo huo, wao Man City wanamfikiria pia Pochettino, wakati ambapo Pep Guardiola akiwa bado hajasaini mkataba mpya.

Ripoti zinasema kwamba, Guardiola hajaonyesha nia ya kutaka kusaini mkataba na klabu hiyo ambapo wa sasa unamalizika msimu ujao.

## KWA UFUPI

**BRUYNE HAMTAKI MESSI CITY**

KIUNGO wa Manchester City, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 29, amesema kuna wachezaji wengi wazuri klabuni hapo na hivyo hakuna haja ya kumsajili straika wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33. ***(Manchester Evening News)***

**WENGER AMTETEA OZIL**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, amesisitiza kiungo Mesut Ozil, mwenye umri wa miaka 31, bado anaweza kuwa na mchango mkubwa kwa 'Washikabunduki' hao. ***(Goal)***

**CASILLAS AMTAJA MOURINHO**

GOLIKIPA wa zamani wa Real Madrid na Hispania, Iker Casillas, amesema kocha wa sasa wa Tottenham, Jose Mourinho alikuwa mtu wa kwanza kumpigia simu baada ya kupatwa na shambulio la moyo akiwa kwenye mazoezi na Porto. ***(ESPN)***

**WOODWARD AMTISHIA SOLSKJAER**

MAKAMU Mwenyekiti wa Manchester United, Ed Woodward, hatasita kumfukuza kazi kocha, Ole Gunnar Solskjaer kama ataendelea kuwa na msimu mbaya. ***(Sunday Mirror)***

**WEST HAM KWA BENRAHMA**

KLABU ya West Ham United imetoa ofa ya pauni milioni 17, ili kumsajili mshambuliaji wa Brentford na Algeria, Said Benrahma, mwenye umri wa miaka 25. ***(90 Min)***

**BALE KUMVUTA RODON SPURS**

STRAIKA aliyejiunga na Tottenham Hotspur kwa mkopo, Gareth Bale, anaweza kuwa na mchango mkubwa wa Spurs kuweza kumsajili mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Wales, Joe Rodon mwenye umri wa miaka 22, anayecheza kule Swansea. ***(Star on Sunday)***

**LIVERPOOL KUMSAJILI BUTLAND**

LIVERPOOL inafikiria kumsajili golikipa wa Stoke City, Jack Butland mwenye umri wa miaka 27. ***(Sunday Mirror)***

**SPURS YAMFUNGUKIA WATKINS**

TOTTENHAM Hotspur ilifanya mazungumzo ya kumsajili Staika, Ollie Watkins, ambaye alikuwa tayari kujiunga na kikosi hicho, kabla ya Mwenyekiti Daniel Levy kughairi baada ya ada iliyotajwa na Brentford ya pauni milioni 28 ili kumpata mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

**HAVERTZ AKIRI EPL NI NGUVU**

KIUNGO wa Chelsea, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21, amesema Ligi Kuu ya England ni ya nguvu zaidi ikilinganishwa na ile ya Ujerumani, Bundesliga. ***(Evening Standard)***

**KEAN HAJUTII KUONDOKA EPL**

STRAIKA wa Everton na Italia, Moise Kean mwenye umri wa miaka 20, amebainisha hajutii kuondoka soka la Uingereza na kwenda Paris St-Germain. ***(Mail on Sunday)***

**LEICESTER NAYO KWA RODON**

KLABU ya Leicester City pia inawania kumsajili Joe Rodon, lakini wao wanataka kuipata huduma yake katika dirisha la Januari ama kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Sun on Sunday)***

**SABABU UNITED KUMKOSA SARR**

OMBI la Manchester United la kutaka kumsajili winga wa Watford, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22, kwa mkopo wa muda mrefu, lilikataliwa kwani walikuwa wanataka kumuuza moja kwa moja. ***(Manchester Evening News)***

**MOWATT SASA LULU ENGLAND**

KLABU za Middlesbrough, QPR na Cardiff City zinamwania kwa karibu mlinzi wa kati wa Barnsley, Alex Mowatt mwenye umri wa miaka 25. ***(Football League World)***

## HABARI MICHEZO



Waratibu wa mbio za Rock City Marathon, Naftal Kasala (wa pili kulia) na Samwel Gisayi (Kushoto) sambamba na wawakilishi kutoka klabu za wakimbiaji wa mbio hizo, Caroline Joseph (wa pili kushoto) na Mustafa Abdulhafidhi (kulia), wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa mbio hizo iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, wakionyesha fulana kwa ajili ya washiriki wa mbio za msimu wa 11 zinazotarajiwa kufanyika Novemba 29, mwaka huu jijini Mwanza. **MPIGAPICHA WETU**

# ROCK CITY MARATHON 2020 SASA ZAZINDULIWA RASMI

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa 11 wa mbio za Rock City Marathon zinazofanyika kila mwaka jijini Mwanza, umezinduliwa rasmi mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Waandaaji wa mbio hizo Kampuni ya Capital Plus International, imesema mbio hizo zenye agenda ya kutangaza utalii wa ndani katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, zimepangwa kufanyika Novemba 29, mwaka huu eneo la Rock City Mall jijini Mwanza.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya uzinduzi huo, Mratibu wa mbio hizo, Kasara Naftal, alisema maandalizi muhimu yameshafanyika ikiwamo suala zima la fulana za washiriki pamoja na medali huku akitaja mbio zitakazohusishwa kuwa ni Km 21, Km 10 na Km 5.

"Kuhusu zawadi, pamoja na medali, washindi wa kwanza wa mbio za kilomita 21 kwa wanaume na wanawake watajinyakulia Sh. milioni mbili kila mmoja, Sh. milioni 1.3 kwa washindi wa pili na Sh. 700,000 kwa washindi wa tatu, huku washindi wanne hadi kumi nao pia wakiibuka na zawadi za medali na pesa taslimu.

"Kwa upande wa mbio za kilomita 10, hatutakuwa na zawadi za fedha taslimu isipokuwa washiriki watajipatia medali na fulana na kuhusu mbio za kilomita tano ambazo zitahusisha washiriki kutoka mashirika na taasisi mbalimbali (corporates) sambamba na washiriki wenye ulemavu wa ngozi (ualbino) zawadi za fedha taslimu zitatolewa kwa washindi watatu," Naftal alifafanua.

Mbio za Rock City Marathon zilizoanzishwa miaka 11 iliyopita, zinazozidi kujiongezea umaarufu kila mwaka na tayari zimefanikiwa kuwavutia baadhi ya wadhamini ikiwa ni pamoja na Kampuni za TIPER, Pepsi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Kampuni ya Ujenzi ya CRJE, Pigeon Hotel, CF Hospital, Hospitali ya Bugando, Garda World, The Cask na Chuo cha SAUT Mwanza.

Kwa upande wa msemaji wa mbio hizo, Samwel Gisayi, alisema usajili wa mbio hizo tayari umeanza kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya mbio hizo pamoja na usajili wa kawaida kupitia vituo mbalimbali vilivyopo mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Arusha huku mikoa zaidi ikiendelea kuongezwa.

"Usajili unaendelea vizuri na mwitikio wa washiriki ni mkubwa. Lengo ni kukimbiza washiriki wasiopungua 3,000 yakiwamo makundi yote yaani wakimbiaji wa mbio za ushindani (Elite runners), washiriki wa mbio za kujifurahisha (Fun run) pamoja na wanafunzi," alisema.

Wakizungumza katika hafla hiyo iliyohusisha wawakilishi wa klabu mbalimbali za wakimbiaji za jijini Dar es Salaam, baadhi ya wakimbiaji waliwapongeza waandaaji wa mbio hizo kwa namna walivyojiandaa huku wakibainisha kuwa maandalizi hayo yanazifanya mbio hizo kuendelea kuwa miongoni mwa mbio kubwa nchini.

"Tumekuwa karibu sana na waandaaji wa mbio hizi na tumejionea wenyewe namna walivyojipanga kuhakikisha mambo yanaenda vizuri zaidi. Tuwatoe hofu washiriki wenzetu hapa kila kitu kipo vizuri kikubwa wajitokeze kwa wingi kuja kushiriki ili pia tupate fursa ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Kanda ya Ziwa ikiwamo Visiwa vya Saanane na Hifadhi mpya ya Burigi Chato," alisema Caroline Joseph mwakilishi wa wakimbiaji pamoja na balozi wa mbio hizo.

## Kipanga kuonyesha cheche Ligi ya Vijana

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa timu ya Kipanga chini ya umri wa miaka 20, Ramadhani Ahmada Idd, amesema msimu huu wamejipanga kufanya vizuri kwa upande wa Ligi ya Vijana ambayo inatarajia kuanza mwezi ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema msimu uliopita licha ya kuwa mara ya kwanza kuchezwa ligi hiyo kwa timu za vijana za timu kubwa za Ligi Kuu Zanzibar, lakini walikuwa miongoni mwa zilizofanya vizuri ingawa ligi hiyo haikumaliza kutokana na mlipuko wa janga la corona.

Alisema msimu huu wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi, hatua itakayowasaidia kuzalisha wachezaji wenye uwezo watakaoitumikia timu ya wakubwa ya Kipanga Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema Ligi ya Vijana ndio pekee ambayo inaweza kuzalisha wachezaji wenye uwezo na nidhamu za wachezaji, hivyo Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) linatakiwa kuisimamia kwa umakini mkubwa ili kufikia lengo lilokusudiwa la kuwapo kwa ligi hiyo ambayo kwa msimu huu itakuwa mara ya pili kuchezwa.

"Dhumuni la kuwapo kwa Ligi ya Vijana kwa kila timu inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, ni wazo zuri ambalo linatakiwa lisimamiwe na kutiliwa mkazo mkubwa, hapa ndipo tutawapata wachezaji tunaowataka na kuwategemea katika timu zetu za Taifa, maana mchezaji wa umri wa chini ya miaka 20 unauwezo wa kumfundisha na akafundishika," alisema

Aidha, aliiomba ZFF kuangalia uwezekano wa ligi hizo kuchezwa siku ambayo timu zao kubwa zinacheza ili kuleta radha ya ligi hiyo ambayo inahudhuriwa na vijana wengi uwanjani.

ZFF katika msimu uliopita wa 20219/2020, ilipanga Ligi ya Vijana kuchezwa siku za mapumziko kutokana na wachezaji wengi wanaocheza timu hizo kubanwa na ratiba za masomo shuleni kwa kuwa ni wanafunzi.

## Kiduku amwanzishia Mthailand dozi kutwa mara tatu

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Twaha Kiduku, amesema anaendelea na mazoezi magumu kutwa mara tatu, asubuhi, mchana na jioni wakati huu akijiandaa kupanda ulingoni dhidi ya mpinzani wake, Sirimongkol Singwancha kutoka Thailand.

Katika pambano hilo ambalo litapigwa jijini Dar es Salaam Oktoba 30, mwaka huu, mabondia hao watakuwa wakiwania mkanda wa dunia uzito wa kati, kilo 76, unaotambuliwa na Baraza la Ngumi Duniani (WBC).

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka mjini Morogoro Twaha alisema enaendela na mazoezi makali katika kambi yake aliyoiweka maeneo ya Mazingu Road sehemu ambayo inampa utulivu wa kutosha kuweza kujifua vizuri.

"Naendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kukutana na mpinzani wangu huyo, lengo ni kuwapa burudani Watanzania siku hiyo," alisema Kiduku.

Alisema tayari amemfuatilia mpinzani wake katika mambano ambayo ameyacheza na anatambua ni bondia mwenye rekodi nzuri ambapo ameshinda mapambano 97 kati ya 101 aliyocheza hadi sasa.

"Nimemfuatilia kwa kipindi kirefu ni bondia mwenye rekodi nzuri ambaye nikikutana naye nitajifunza mambo mengi," alisema.

Kuhusu mazoezi, alisema amekuwa akijifua kila siku asubuhi mchana na jioni, akiwa chini ya walimu wake Pawa Ilanda pamoja na Saimon Mponela.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Kiduku, Ilanda alisema, anamjenga zaidi kisaikolojia pamoja na kumpa mazoezi ya kumjenga mwili anaamini atafanya vizuri kwa kuwa kila mchezo kwao wanauchukulia kama fainali.

Alisema licha ya Mthailand huyo kuwa na rekodi nzuri, hana wasiwasi kwa kuwa mara nyingi wakikutana na bondia kutoka nje ya nchi pambano huwa linakuwa jepesi kwao.

"Nimemfuatilia bondia huyo wa Mthailand, anatumia akili nyingi akiwa ulingoni na ana nguvu sana, hivyo ninampa mazoezi ambayo naamini atafanya vizuri," alisema Ilanda.

**MSHINDI...**




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Aldofu Chanda, kutoka Iringa akionyesha mfano wa hundi ya Sh. 10,619,725 baada ya kukabidhi kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya mechi za mpira wa miguu wiki iliyopita. Jackpot ya SportPesa wiki hii ni Sh. 225,116,840. **PICHA: SPORTPESA**

Michezo
Jumatatu Oktoba 12, 2020
Nipashe



POCHETTICHO SASA LULU KWA MAN UNITED, CITY

HABARI UK 22

MSITU...



Winga wa Taifa Stars, Simon Msuva, akimiliki mpira huku 'msitu' wa mabeki wa timu ya Taifa ya Burundi wakiwa wamejipanga vema kumkabili wakati wa mchezo wa kirafiki wa kimataifa ulipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana na wageni hao kushinda kwa bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MORRISON, MIQUISSONE WAANIKWA SIMBA SC

## Yasema Mghana huyo hurahisisha maisha kambini, Kamati TFF nayo kumjadili leo, huku mwenzake...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KLABU ya Simba imewachambua wachezaji wao wanaocheza winga ya kulia na kushoto, Luis Miquissone raia wa Msumbuji na Mghana Benard Morrison kuwa licha kuwa na vipaji vikubwa kwenye kusakata soka, lakini kuna kitu kikubwa kinachowatofautisha ambacho ni tabia zao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Meneja wa klabu hiyo, Patrick Rweyemamu baada ya mazoezi ya utimamu wa mwili 'gym', alisema pamoja na wote kuwa mahiri kwenye kusakata kambumbu, lakini Miquissone yeye kitabia ni mpole sana na si mtu wa kujichanganya kama mwenzake Morrison ambaye ni mcheshi.

"Luis ni mtulivu, si mchangamfu sana, siyo mtu wa kujichanganya sana, nadhani maisha aliyokulia hayakuwa ya kujichanganya, pia inaonekana ndiyo hulka yake." alisema meneja huyo na kumwelezea Morrison kuwa yupo tofauti na mwenzake.

"Yeye Morrison ni mtu wa kujichanganya, mcheshi, kila tukio yupo, pia ni mchekeshaji yaani 'komediani', na hii inasababisha maisha ya kambi yawe rahisi kwa wenzake na watu wengine kwa ujumla," alisema meneja huyo.

Miquissone alisajiliwa na Simba katikati ya msimu uliopita wa Ligi Kuu, kipindi cha dirisha dogo akitokea UD Songo ya Msumbiji alikokuwa akicheza kwa mkopo kutoka Mamelodi Sundowns, huku Morrison akisajiliwa usajili wa dirisha kubwa baada ya kumaliza mkataba na Yanga.

Kuhusu kuahirishwa kwa mechi ya watani wa jadi, Rweyemamu alisema kuwa imevunja morali ya wachezaji wake kwani walikuwa wamejiandaa sana na mechi hiyo.

"Nikwambie ukweli imetuathiri kisaikolojia kwa sababu tulijiandaa kweli kweli. Mimi sisemi kwa ushabiki, lakini nakwambia tulijiandaa hasa, kwa hiyo sasa tunajiandaa na mechi zingine, lakini imetupa muda wa kuendelea na mazoezi na hii itatupa muda wa kuendelea kujiandaa zaidi ya mara mbili au tatu ya mwanzo kwenye mchezo wa 'dabi'," alisema.

Katika hatua nyingine Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) inatarajia kukutana leo kujadili mambo mbalimbali ikiwamo mbivu mbichi juu ya malalamiko ya Yanga iliyoyatoa kuhusu kasoro zilizopo kwenye mkataba wa Morrison na Simba.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili kutoka ndani ya chanzo chetu katika kamati hiyo zilieleza kuwa inatarajia kukutana leo kwa ajili ya kupitia malalamiko hayo.

"Kamati inakutana leo, hukumu na ukweli juu ya Yanga kuhusu mkataba wa Morrison na Simba kuwa na makosa, itajulikana baada ya kikao hicho," kilieleza chanzo chetu.

Hivi karibuni uongozi wa Yanga uliibua upya sakata la winga huyo kwa kudai kuwa mkataba wake mpya alioingia na Simba hauna saini za kiongozi yeyote wa mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kauli hiyo Yanga ilikuja baada ya kamati hiyo ya TFF kumtangaza Morrison kuwa ni mchezaji huru katika kesi yao ya awali ya kimkataba na baadaye kusajiliwa na Simba, lakini klabu yake hiyo ya awali ikieleza kuwa imewasilisha rufani yao Mahakama ya Usuluhishi ya masuala ya Soka (CAS) hata hivyo kabla ya majibu hayo kutoka ndipo ikaibuka na sakata jipya la mapungufu yaliyopo katika mkataba wa mchezaji huyo na Simba.

# TAIFA STARS KICHWA CHINI NYUMBANI

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na Said Ntibazonkiza dakika sita kabla ya mechi kumalizika, liliifanya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kuondoka kichwa chini nyumbani kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Burundi, 'Intamba Murugamba.'

Katika mechi hiyo ya kirafiki ya kimataifa iliyo kwenye Kalenda ya FIFA, ambayo iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, mfungaji aliupata mpira akiwa mbali kidogo na eneo la hatari, lakini alipiga shuti la juu la pembeni lililomuacha kipa David Kissu akiruka bila mafanikio.

Taifa Stars inabidi ijilaumu yenyewe kwa kukosa japo kutoka sare kwenye mechi hiyo kutokana na kukosa magoli mengi katika mchezo huo ambao iliumiliki kwa asilimia kubwa.

Dakika ya tano tu ya mchezo, Idd Nado aliingia kwenye eneo la hatari na kupiga shuti kali ambalo lilipaa juu ya lango la Burundi huku Warundi hao nao nusura wapate bao baada ya Cedric Amissi kuukuta mpira uliotemwa na kipa Kissu, lakini shuti lake lilitoka nje kidogo ya lango.

Nahodha wa Stars, Mbwana Samatta aliikosesha timu yake bao dakika ya 18 akiwa anatazamana ana kwa ana na kipa wa Burundi, lakini shuti lake lilipaa juu la lango.

Dakika ya 50 pia Simon Msuva akiwa peke yake na kipa akapiga mpira uliogonga nguzo huku Shomari Kapombe, Nado, na Said Ndemla wakikosa magoli ya wazi dakika ya 52, 56, na 79.

Stars ilipata pigo dakika ya 75 wakati kiungo wake Jonas Mkude alipozawadiwa kadi nyekundu, ikiwa ni njano ya pili kutokana na kumchezea vibaya mchezaji Fredrick Nsengiyuva wa Burundi.

Kutoka kwa Mkude kulionekana kuipa nguvu Burundi, kwani ndipo walipoanza kuutawala mchezo na kufanya mashambulizi kadhaa ambayo yalisababisha kupata bao hilo pekee.

Kwenye mechi hiyo Stars iliwatoa Ndemla, Samatta, Feisal Salum na Abdallah Kheri na nafasi zao zikichukuliwa na Mzamiru Yassin, Thomas Ulimwengu, Ditram Nchimbi na Salum Aboubakar, mabadiliko ambayo hayakuweza kubadili ubao wa magoli.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002